Jumanne Julai 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581375

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

## Mkakati wasukwa ajali za barabarani, wakuu trafiki mikoa, wakaguzi wanolewa

UKURASA 3




## Rais Hungary kuzuru nchini kikazi siku 4

UKURASA 2




UKURASA 11

# Jicho la Samia, JK demokrasia Afrika

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali kabla ya kufungua Mkutano wa Jukwaa la Demokrasia Afrika uliofanyika jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

## PPRA yabaini vigingi vinane ununuzi

UKURASA 3

## BoT yaja na kanuni malipo ya fedha za kigeni hotelini



UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

### CHADEMA YAJIWEKA KANDO MABADILIKO SHERIA YA UCHAGUZI

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema hakiko tayari kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi, kikisisitiza msingi wa tatizo uko katika Katiba ya Jamhuri ya ...

**MICHEZO** MAYELE AVUTA WANNE YANGA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA




Wanafunzi wakifanya udahili katika banda la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kwenye Maonesho ya 18 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jicho la Samia, JK demokrasia Afrika

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mbegu inayopandwa na viongozi wa bara la Afrika katika kuimarisha demokrasia, ndio msingi wa hekima na ujenzi wa Afrika inayotarajiwa pamoja na kufikia malengo Agenda 2063 yenye kuitaka Afrika kuwa yenye amani, maendeleo na utangamano.

Mbali na hilo, Rais Samia amesema kunahitajika mikakati kwa kuwa takwimu zinaonesha kwa kipindi cha miaka minane iliyopita, bara limekuwa si salama kutokana na migogoro katika kanda kadhaa ikiwamo magharibi na mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Arusha alipofungua mkutano wa wadau wa demokrasia Afrika ulioshirikisha viongozi walioko madarakani na waliostaafu barani.

"Ni imani yangu mkutano huu utaendelea kufanyika hapa (Tanzania). Mkutano huu umejawa na hekima, tupo hapa kujifunza kutoka kwa viongozi wetu... kwa Kiswahili kuna msemo usemao, palipo wazee hapahariibiki jambo," alisema Rais Samia.

Alisema katika kuimarisha demokrasia, alianzisha mazungumzo ya pamoja na vyama vya upinzani ili kulinda amani na mustakabali wa taifa kidemokrasia na aliunda Tume ya Haki Jinai kwa lengo la kuimarisha demokrasia na tayari tume hiyo imekabidhi ripoti na imeanza kujadiliwa.

"Demokrasia ina uhusiano mkubwa na amani, jamii yenye ustawi na maendeleo ya kijamii. Tunaoamini kwamba demokrasia ni chanzo cha maendeleo... demokrasia ili iwe na maana inapaswa kuimarisha huduma za kijamii," alisema Rais Samia.

"Watu ndio wahusika wakuu katika mfumo wa kidemokrasia na utawala. Hali isiyo nzuri ya kiuchumi kwa baadhi ya nchi za bara hili, imekuwa chanzo cha kutotimizwa huduma na kulinda haki, kutokana na uchumi usio sawa.

Awali, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, alisema bara la Afrika linakabiliwa na migogoro ya kisiasa, vita, mabadiliko ya tabianchi ikiwamo janga la UVIKO-19, kupanda kwa bei za vyakula na nishati na vita vya Russia na Ukraine vilivyoathiri kwa kiwango kikubwa maendeleo ya bara.

"Kama kiongozi mstaafu, ninaweza kusema kuwa kiongozi wa Afrika ataelezea changamoto hizo kwa sababu ni wajibu wake pia katika kutatua. Afrika ni bara pekee lenye mipaka ambayo imenyooka kana kwamba siyo ya asili, yaani mpaka umenyooka tu mnakubaliana upande huu wako na wewe huku, siyo kama mabara mengine duniani," alisema Kikwete.

Alisema kuna uhamasishaji wa uongozi shirikishi na kutoa vipaumbele kwa baadhi ya maeneo, ingawa hatua za utekelezaaji hutegemea na nchi na nchi, bara na bara katika ajenda ya ujenzi wa demokrasia.

"Kila nchi ina hadithi yake ya kusimulia. Ninaweza kuthubutu kwa kujiamini, sisi Tanzania tuna bahati, shukrani kwa waanzilishi wa taifa hili, Mwalimu Julius Nyerere - Rais wa Kwanza wa Tanganyika na Shekhe Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar, ambao walijenga misingi imara na mafanikio makubwa kwa viongozi nikiwamo mimi," alisema.

Kikwete alisema hivi sasa Tanzania ikiwa na watu milioni 61 na taifa lenye kujivunia, ina makabila tofauti yapatayo 126 na viongozi tofauti wa kisiasa.

"Tuna takribani vyama vya kisiasa 24 lakini tuna amani miongoni mwetu. Tupo vizuri sasa kuliko awali ila tunahitaji kufanya zaidi katika demokrasia. Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na serikali yako, mpo kwenye hatua inayoridhisha katika hili ingawa kunahitajika kufikia makubwa zaidi, tafadhali endelea kufanya kazi kubwa kama vile kaulimbiu yako ya 'Kazi Iendelee,'" Kikwete alisema.

Kiongozi huyo alisema migogoro barani Afrika inayoshuhudiwa sasa, inatokana na uongozi. Aliitaja ni hali isiyokubalika. Kunahitajika mabadiliko kwa kuwa inawezekana.

**ZIARA YA RAIS**

Katika hatua nyingine, mwandishi wetu Elizabeth Zaya anaripoti kuwa Rais wa Hungary, Katalin Novak, jana aliwasili nchini kwa ziara ya kikazi.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, ziara hiyo ni matokeo ya jitihada za Rais Samia kuimarisha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine.

Taarifa ya Waziri ilisomwa kwa niaba yake na Balozi Mindi Kasiga, akieleza kuwa ziara hiyo inatokana na sera mpya ya Hungary kwa nchi za Afrika inayolenga kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi.

"Uhusiano wa Tanzania na Hungary umekuwa mzuri tangu enzi za Muungano wa Soviet na kupitia ziara hii, tunatarajia uhusiano huo kuimarika zaidi hususani katika uwekezaji, biashara na utalii ambapo takwimu katika maeneo hayo haziridhishi sana," alisema.

Alibainisha kuwa leo rais huyo atapokewa Ikulu na Rais Samia na kushiriki mazungumzo ya faragha na baadaye mazungumzo rasmi na kufanya mkutano na waandishi wa habari kisha viongozi hao watashiriki dhifa ya chakula cha mchana.

Rais Katalin anatarajia kutembelea ofisi za Ubalozi wa Heshima wa Hungary nchini uliopo Kawe, Dar es Salaam na kesho atasafiri kuelekea jijini Arusha kwa ziara binafsi na kurejea Hungary keshokutwa kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

## BoT yaja kanuni mpya malipo ya fedha za kigeni hotelini

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeanzisha kanuni mpya zinazolenga kuweka utaratibu utakaowezesha hoteli za kitalii nchini kutoa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni kwa wateja wao.

Hatua hiyo imetokana na hoteli hizo kupokea idadi kubwa ya wageni wanaofanya malipo kwa fedha za kigeni, utaratibu utakaowezesha serikali kujua takwimu sahihi za fedha za kigeni.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao na wadau wa biashara ya ubadilishaji fedha za kigeni.

Tutuba alisema BoT kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikutana na wadau wa sekta ya hoteli Zanzibar Januari mwaka huu na kujadili namna ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni katika maeneo ya hoteli za kitalii.

Alisema ilibainika wamiliki wa hoteli wanapokea fedha nyingi za kigeni kupitia wageni wanaofanya malipo ya kulala, hali inayoinyima serikali kufahamu takwimu sahihi za fedha za kigeni.

"Mmiliki wa hoteli akipokea fedha za kigeni anakwenda kuzibadilisha ili alipe mishahara, anunue bidhaa. Hivyo, baada ya kanuni mpya mmiliki wa hoteli akishapokea fedha hizo, atatakiwa kuzisajili, atatoa taarifa kwa serikali, kisha ataziweka kwenye akaunti yake (benki), serikali itaziona. Lengo tujue takwimu za fedha za kigeni," alisema Tutuba.

Alisema pamoja na marekebisho ya kanuni hizo, BoT inaendelea kuhamasisha benki na taasisi za fedha kuboresha utoaji huduma ya kubadilisha fedha za kigeni.

Tutuba alisema hadi Juni mwaka huu, benki za biashara 37 zenye mtandao wa matawi zaidi ya 900 nchi nzima zimeendelea kutoa huduma hizo.

Alisema maduka manane ya kubadilisha fedha yenye matawi 36 nchini yalikuwa yamepewa leseni.

Tutuba alitaja sababu za kuadimika kwa dola za Marekani nchini zinajumuisha kuongezeka mahitaji ya dola kutokana na uchumi kufunguka baada ya janga la ugonjwa wa corona.

Alitaja sababu nyingine ni vita kati ya Urusi na Ukraine vilivyosababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali ikiwamo usafirishaji, hivyo kuongeza mahitaji ya dola.

Tutuba alitaja sababu nyingine ni mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mahitaji makubwa zaidi ya dola pamoja na sera ya fedha ya Marekani (kupandisha riba) iliyovutia wawekezaji wengi kuwekeza dola zao Marekani na kusababisha uhaba duniani.

Alisema BoT imeendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upatikanaji wa dola na sarafu zingine za kigeni na kuchukua hatua stahiki kuhakikisha uchumi wa nchi hauathiriwi sana na changamoto hiyo.

Alisema kuwa hadi Julai 14 mwaka huu, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ni dola za Marekani bilioni 5.55, kiasi kinachokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi mitano.

# Mkakati wasukwa ajali barabarani

## -Wakuu trafiki, wakaguzi magari wajifungia

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi limetoa maagizo tisa kwa wakuu wa usalama barabarani wa mikoa na wakaguzi magari, ikiwamo kudhibiti rushwa na muhari kwa madereva wazembe, ili kupungua ajali za barabarani nchini.

Maagizo hayo yalitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa jeshi hilo, Awadhi Haji Awadhi, alipozindua mafunzo kwa wakuu wa usalama barabarani wa mikoa na wakaguzi magari nchini.

Kwa mujibu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, jumla ya watu 886 walipoteza maisha katika kipindi cha kati ya Januari na Novemba mwaka jana (2022) kutokana na ajali za barabarani.

Vilevile, watu 573 walipata majeraha kutokana na ajali 1,422 zilizorekodiwa na kikosi hicho kwa kipindi tajwa. Ni ongezeko la ajali 11 kulinganisha na zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2021 zilizosababisha vifo vya watu 1,008 na kujeruhi 1,496.

Katika uzinduzi wa mafunzo hayo ya siku tatu kwenye Ukumbi wa Kampuni ya Superdoll iliyoyafadhili, Kamishna Awadhi aliagiza maarifa na mafunzo hayo yasaidie kupunguza ajali za barabarani.

Alielekeza kila mshiriki akasimamie vizuri sheria na taratibu zilizopo ili kila anayeendesha gari azizingatie.

"Muhari na madereva wazembe uachwe. Dereva anakutwa anaendesha amelewa anapewa adhabu hafifu, anakwenda kurudia makosa. Madereva wazembe wafutiwe leseni kwa mujibu wa sheria, bila kupepesa macho, bila kumwonea mtu," aliagiza.

Kamishna Awadhi aliwaagiza maofisa hao kuweka mpangokazi unaolenga kupambana na ajali za barabarani nyakati zote, ikizingatiwa serikali imetoa rukhsa mabasi kusafirisha saa 24.

Katika agizo lake la tatu, Kamishna Awadhi aliwataka maofisa hao kupiga vita rushwa, akisisitiza "...lazima mkadhibiti vitendo vya rushwa. Ninyi wenyewe msichukue wala kuomba rushwa kwa askari mnaowaongoza. Pia mchukue hatua kwa kuwawajibisha wanaojihusisha na rushwa. Rushwa ni chanzo cha ajali za barabarani." "Leseni za udereva zitolewe kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Asiyekidhi sifa asipewe leseni, hata kama ni shangaza yako, hata kama ni mwanao. Akiingia barabarani atasababisha kifo na majeraha kwake na wengine.

"Mkazingatie nidhamu na maadili ya kazi. Maadili yaongozwe na maarifa mtakayopata hapa," alisema Kamishna Awadhi huku akiagiza pia kufanyike doria katika barabara kuu zote kuhakikisha watumishi wanazingatia sheria za usalama barabara.

Kiongozi huyo pia aliagiza kuwe na usimamizi wa sheria bila woga na uonevu, ikiwamo kwa mabasi ambayo madereva wake wanashindana barabarani.

"Kuwe na operesheni za kukamata magari mabovu, ili mwisho wa siku kuwe tu na magari yanayostahili kuwapo barabarani," aliagiza Kamishna Awadhi na kuwataka watendaji hao kuwa na ushirikiano na wadau aliowataka LATRA, TIRA, TRA na wengineo katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

Awali, Mwenyekiti wa Kampuni ya Superdoll Seif Ally alisema lengo la kuandaa mafunzo hayo ni kuunga mkono jitihasda za serikali katika kukabiliana na ajali za barabarani zinazogharimu maisha ya watu wengi nchini.

Alisema Tanzania ni nchi salama kiulinzi lakini haiko salama kwa ajali za barabarani, akieleza kuguswa na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuchoshwa na ajali hizo.

Alisema kuwa licha ya mafunzo hayo kugharimu fedha nyingi, wameona kuna haja kuyatoa kwa maofisa hao wa Jeshi la Polisi ili kukabiliana na ajali nchini, wakileta pia wataalamu kutoka nje.

Seif alisema kuwa ili nchi iwe salama dhidi ya ajali barabarani, kunahitaji kufanyike mambo matatu: utii wa sheria na kanuni; mafunzo endelevu; na kuwekeza katika teknolojia na ubunifu.

Maofisa 119 wa Jeshi la Polisi wanashiriki mafunzo hayo.

# PPRA yaona vigingi vinane katika ununuzi wa umma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imebaini vikwazo vinane vinavyoukabili ununuzi wa umma kwa taasisi za ununuzi na wazabuni, ikiwamo kukithiri kwa vitendo vya rushwa na uwazi usioridhisha katika mchakato wa zabuni.

Kutokana na hilo, serikali inakusudia kufanya maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na kutofumbia macho mtumishi yeyote atakayebainika kwenda kinyume cha taratibu zilizopo za ununuzi.

Akieleza utekelezaji wa majukumu ya taasisi na mwelekeo wa mwaka 2023/24 jana kwa waandishi wa habari jijini hapa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi, alisema uwazi usioridhisha unasababisha kutopatikana taarifa za zabuni, thamani ya mkataba na ukosefu wa uaminifu.

Alisema ununuzi wa umma unakabiliwa na hatari kubwa ya rushwa kutokana na watendaji na maofisa serikalini kulalamikiwa na kuhisiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa kutoa mikataba au kuwapa faida zisizo halali wazabuni wasio na sifa.

"Kuna kikwazo cha mchakato wa zabuni kuchukua muda mrefu. Hili ni takwa la kisheria kufuata taratibu na kanuni za ununuzi wa umma ikiwa ni pamoja na kufuata sheria za ushindani na taratibu zingine zinazohusiana nazo. Hatua hizi za kisheria mara nyingi huongeza muda wa mchakato, hivyo watumishi wasio waadilifu wanakuwa sababu ya zabuni kuchukua muda mrefu," alisema.

Alibainisha kutozingatia taratibu za ununuzi wa umma ambapo kuna ukiukwaji wa taratibu na miongozo na hivyo kusababisha upendeleo kwa kampuni zisizostahili, kutokuwapo ushindani na matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Pia wazabuni kuwasilisha bidhaa au huduma zisizoridhisha au zilizo chini ya viwango, bei za bidhaa kubwa kuliko uhalisia wa bei za soko, wazabuni wasiokuwa na uwezo kuomba zabuni na kushawishi kwa kutoa rushwa.

Akizungumzia mwelekezo wa serikali katika kukabiliana na vikwazo hivyo, alisema PPRA imekusudia kufanya maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, ili kukidhi mahitaji ya wateja yaliyoko sokoni ikiwa ni pamoja na kuondoa urasimu usiokuwa wa lazima na kuongeza uwajibikaji kwa wale wote wanaojihusisha na ununuzi wa umma.

"Pia kupunguza siku za mchakato wa ununuzi ili kupunguza muda unaotumika katika mchakato wa ununuzi wa umma na kuongeza ufanisi katika kutekeleza miradi na kuwekeza kwenye kulinda uadilifu wa mfumo wa ununuzi wa umma kupitia kuwapo miongozo maalum ya ununuzi," alisema.

Akizungumzia mfumo mpya wa ununuzi kwa njia ya mtandao (NeST), Maswi alisema kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, mfumo umeanza kutumika rasmi.

Pia alisema ifikapo Oktoba Mosi, mwaka huu taasisi za serikali hazitoweza kutuma mialiko ya zabuni katika mfumo wa TANePS na badala yake zitapaswa kutumia mfumo wa NeST.

"Kwa kipindi cha kuanzia Julai mosi, 2023 mpaka 30, Septemba 2023, Mfumo wa TANePS hautapokea malipo ya ada za usajili mpya kwa wazabuni, malipo yatakayopokelewa kwa kipindi hicho ni ada za kutangaza zabuni na ada ya kuomba zabuni," alisema.

Alisema zabuni zitakazoruhusiwa kutangazwa katika Mfumo wa TANePS kwa kipindi hicho ni zabuni za muda mfupi tu pamoja na bidhaa mtambuka ambazo mchakato wake wa kupata mshindi utakuwa umekamilika kabla au Desemba 31, 2023.


**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**COMMERCIAL CASE NO. 77 OF 2022**

**FURNITURE CENTRE (DAR ES SALAAM) LIMITED................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**PLUS NETWORKS TANZANIA LIMITED...........................DEFENDANT**
**DECREE**

**WHEREFORE,** the Plaintiff, **FURNITURE CENTRE (DAR ES SALAAM) LIMITED**, by way of a plaint, instituted this suit against the defendant praying for judgment and decree as follows;

(i) For payment of TZS 92,761,656 being the total outstanding amount for supply of various types of furniture.
(ii) For payment of the agreed interest on the outstanding amount at the rate of 3% per months computed from the dates the payment fell due to the date of filing this suit.
(iii) For payment of interest at the commercial rate prevailing at the date of judgement, or at such rate as the honorable court may deem fit and just accruing and computed from the date of filing the suit to the date of judgement on the outstanding amount of TZS 92,761,656.
(iv) For payment of Tanzania shillings 15,000,000.00 as specific damages arising from the loss of profit during the period which the defendant withheld payment from the plaintiff.
(v) For payment of the general damages as may be assessed by the court.
(vi) For payment of legal fees, expenses, other resultant costs and expenditure incurred by the plaintiff as a result of defendant's breach and actions;
(vii) For payment of any other costs, loss or liability incurred by the plaintiff due to defendant's actions.
(viii) For payment of costs of this suit; and
(ix) Any other relief (s) as the Honorable Court may deem fit and just to grant.

This matter coming up for default judgment on this 10th day of July, 2023 before Hon. A. A. Mbagwa, Judge in the presence of Edgar Nditi, learned advocate for the plaintiff and in absence of the defendant

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT: -**
Judgment and decree are hereby entered against the defendant, **PLUS NETWORKS TANZANIA LIMITED** as follows;
(i) Payment of TZS. 92,761,656 being the total outstanding amount for supplied furniture.
(ii) Payment of the agreed interest on the outstanding amount of TZS. 92,761,656 at the rate of 3% per month computed from the dates the payment fell due to the date of filing this suit.
(iii) Payment of interest on the decretal sum of TZS. 92,761,656/= at the commercial rate of 10% from date of filing the suit to the date of judgement.
(iv) Payment of TZS 5,000,000/= say Tanzania shillings five million being the general damages
(v) Payment of costs of this suit;
(vi) In terms of Rule 22 (2) of the High Court (Commercial Division) Procedure Rules, the plaintiff is ordered to publish the decree at least in two newspapers of wide circulation in the country within ten (10) days from the date of this judgment.

Given under my hand and Seal of this Court on this 10th July, 2023.

A.A. MBAGWA
JUDGE
10/07/2023

TANGAZO

# Tanzania Commercial Bank

Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa 30.06.2023 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31.03.2023 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 53,615 | 53,016 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,634 | 81,056 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 143,237 | 124,814 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 99,319 | 59,605 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 512 | 248 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 117,459 | 141,652 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 837,161 | 858,295 |
| | 12 | Mali Nyingine | 41,797 | 43,222 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 20,593 | 20,511 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,327,327** | **1,382,419** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 870,917 | 919,076 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 172,011 | 113,407 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 7,206 | 2,537 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | (0) | (0) |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 18,850 | 21,369 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 2,547 | 2,641 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 32,028 | 29,473 |
| | 28 | Madeni | 100,429 | 145,959 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,203,989** | **1,234,461** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **123,338** | **147,958** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 31,372 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 74,499 | 73,656 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 7,773 | 2,393 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 40,537 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **123,338** | **147,958** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 161,863 | 157,474 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 29,607 | 78,024 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,856 | 17,703 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 2,396 | 2,396 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.29% | 10.70% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.46% | 8.83% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82.16% | 85.56% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 63.07% | 62.09% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82.71% | 81.36% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 1.01% | 4.59% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -3.99% | 7.17% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya mwaka sasa 30-Jun-23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 36.427 | 34.631 | 71.266 | 69.353 |
| 2 Gharama za Riba | (13.133) | (11.971) | (25.991) | (22.575) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **23,294** | **22,660** | **45,275** | **46,778** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (155) | (40) | (165) | (55) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3.100) | (3.433) | (5.507) | (6.914) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **12.290** | **8.311** | **21.158** | **16.215** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya | 2.893 | 1.199 | 4.534 | 2.622 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 5.091 | 4.732 | 10.301 | 8.871 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 4.306 | 2.381 | 6.323 | 4.722 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(25,211)** | **(24,138)** | **(49,967)** | **(48,811)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 12.224 | 12.146 | 25.078 | 24.492 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 2.376 | 1.819 | 4.108 | 3.373 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 10.612 | 10.174 | 20.781 | 20.946 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **7,118** | **3,360** | **10,795** | **7,212** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1.737 | 1.521 | 3.022 | 3.493 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **5.380** | **1.839** | **7.773** | **3.719** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa** | **5.380** | **1.839** | **7.773** | **3.719** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1.067 | 1.093 | 1.067 | 1,093 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 172 | 66 | 248 | 132 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 52 | 48 | 52 | 48 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.39% | 0.15% | 0.57% | 0.31% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.42% | 1.58% | 6.24% | 3.21% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 51.75% | 56.21% | 54.06% | 57.04% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.12% | 2.25% | 4.11% | 4.71% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-23 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 7.118 | 3.677 | 10.795 | 7.212 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 5.943 | 4.977 | 11.163 | 12.201 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 9.678 | (16.704) | (40.375) | (56.292) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 10.446 | 45.312 | 55.758 | 100.108 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1.014 | (3.029) | 3.273 | (11.183) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1.425 | (3.251) | 994 | (7.465) |
| - Kodi Iliyolipwa | (1.737) | (1.285) | (3.022) | (3.493) |
| - Mengineyo (bainisha) | (8.956) | (22.359) | (41.650) | (23.627) |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **24,930** | **7,338** | **(3,064)** | **17,461** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1.308) | (611) | (1.919) | (1.914) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | - | - |
| Mengineyo (fedha iliyotolewa na serikali) | (30.000) | 30.000 | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(31,308)** | **29,389** | **(1,919)** | **(1,914)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (999) | (1,395) | (2,394) | (2,798) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(999)*** | ***(1,395)*** | ***(2,394)*** | ***(2,798)*** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (7,377) | 35,332 | (7,377) | 12,749 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **123,127** | **87,795** | 123,127 | **144,937** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 115,750 | 123,127 | 115,750 | 157,687 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **31,372** | - | **74,932** | **(0)** | **0** | **9,694** | **115,998** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 7,773 | **7,773** |
| Mapato mengineyo | - | - | (431) | - | - | (3) | **(434)** |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | | | 844 | (844) | | | |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo(Fedha iliyotolewa na serikali) | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **75,346** | **(844)** | **0** | **17,464** | **123,338** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 3,152 | - | - | - | **3,152** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hisa za ziada(Issued bonus shares) | **3,667** | - | **(3,667)** | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo(Kodi ya Hisa za ziada-W/t on bonus share) | **(367)** | | | | | - | **(367)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **74,932** | **(0)** | **0** | **9,694** | **115,998** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI, 2023

Benki ililipa faini ya shilingi 10,000,000/=kutokana na kuchelewesha malipo ya Lombard na shilingi 20,000.00 kutokana na upungufu wa fedha zilizopelekwa Benki kuu(Bot counter shortage) Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| SABASABA K. MOSHINGI **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | Imesainiwa | 17.07.2023 |
| REGINA E. SEMAKAFU **(Mkuu wa Fedha)** | Imesainiwa | 17.07.2023 |
| SOSTHENES F. NYENYEMBE **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | Imesainiwa | 17.07.2023 |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| DR. EDMUND B. MNDOLWA **Mwenyekiti wa Bodi** | Imesainiwa | 17.07.2023 |
| MS. ANNE C. MBUGHUNI **Mjumbe wa Bodi** | Imesainiwa | 17.07.2023 |

217501502

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

# TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES 2023

*All charges are VAT exclusive.

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | MINIMUM OPERATING BALANCE | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | 7,000.00 | 5.00 | 50,000.00 | 100.00 |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | FREE | N/A | 50,000.00 | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | 1,800.00 | 0.86 | 20,000.00 | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | 1,800.00 | N/A | 0 | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000.00 | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | FREE | FREE | 50,000.00 | N/A |
| Platinum Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 5,000 | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | FREE | N/A | 20,000 | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 0 | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000 | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | FREE | N/A | 30,000 | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | 1,800.00 | N/A | 10,000 | N/A |
| Wadu Account | FREE | N/A | FREE | FREE | 10,000 | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | 700.00 | N/A | 1,500.00 | N/A |

## CASH SERVICES

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Cash deposit | | FREE |
| Cash withdrawal TZS | 0 - 100,000 | 3,000 |
| | 100,001 - 400,000 | 3,000 |
| | 400,001 - 500,000 | 4,400 |
| | 500,001 - 800,000 | 4,400 |
| | 800,001 - 1,000,000 | 5,200 |
| | 1000,001- 1,200,000 | 5,200 |
| | 1000,001 - 2,000,000 | 6,100 |
| | 2000,001 - 3,000,000 | 6,100 |
| | 3000,001 - 5,000,000 | 6,100 |
| | 5000,001 - 10,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 1000,0001 - 15,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 1500,0001 - 25,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 25,000,000 - 50,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 50,000,000 - 100,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 100,000,001 - Above | 0.12% - 170,000 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| **BANK STATEMENT** | **TZS** | **USD** |
| Balance enquiry over the counter | 2000.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| **CHEQUE SERVICE** | **TZS** | **USD** |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

## AGENT BANKING SERVICE

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 5,000, 000.00 | 10,000.00 |
| | 5,000,000.01 - 6,000,000.00 | 11,000.00 |
| | 6,000,000.00 - 7,000,000.00 | 12,000.00 |
| | 7,000,000.00 - 8,000,000.00 | 13,000.00 |
| | 8,000,000.00 - 9,000,000.00 | 14,000.00 |
| | 9,000,000.00 - 10,000,000.00 | 15,000.00 |
| Balance Enquiry | | 300.00 |
| Mini Statement | | 300.00 |

## POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Registration | | FREE |
| Transfer Bank to MNO | 0-9,999.99 | 1,100.00 |
| | 10,000 - 19,999.99 | 2,000.00 |
| | 20,000 - 29,99.99 | 2,500.00 |
| | 30,000 - 39,999.99 | 3,200.00 |
| | 40,000 - 49,999.99 | 3,400.00 |
| | 50,000 - 99,999.99 | 4,100.00 |
| | 100,000 - 199,999.99 | 4,800.00 |
| | 200,000 - 249,999.99 | 5,500.00 |
| | 250,000 - 299,999.99 | 6,000.00 |
| | 300,000 - 399,999.99 | 6,500.00 |
| | 400,000 - 699,999.99 | 7,100.00 |
| | 700,000 - 799,999.99 | 8,400.00 |
| | 800,000 - 999,999.99 | 9,500.00 |
| | 10,000,000 - Above | 11,000.00 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

| LOANS | CATEGORY | RATE |
|---|---|---|
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 20,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Application fee | TZS 20,000.00 |
| | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 20,000.00 Maximum TZS 150,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan Application fee | TZS 150,000.00 |
| | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 150,000.00 |
| Charges on Business Loan | Loan Applicationfee for Business Loans | TZS 200,000.00 |
| | Loan Administration fee- Business and Personal loans | 2% of the Approved Amount |

| DORMANT ACCOUNT | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

## POPOTE ATM SERVICE

| ACTIVITY | BAND [TZS] | New Charge (TZS) |
|---|---|---|
| 1. ATM Cash Withdraw | 1,000 – 99,000 | 1,500 |
| | 100,000 – 400,000 | 1,700 |
| 2. Interbank transfer on ATM | 1 – 99,999 | 1,300 |
| | 100,000 - 199,999 | 1,700 |
| | 200,000 - 299,999 | 1,700 |
| | 300,000 - 399,999 | 1,700 |
| | 400,000 - 499,999 | 2,500 |
| | 500,000 - 599,999 | 3,000 |
| | 600,000 - 699,999 | 3,500 |
| | 700,000 - 999,999 | 4,000 |
| | 1,000,000 - 1,999,999 | 5,000 |
| | 2,000,000 - 2,999,999 | 6,000 |
| | 3,000,000 - 3,999,999 | 7,000 |
| | 4,000,000 - 4,000,000 | 8,000 |
| 3. Intra-Bank Transfer on ATM | Any Amount | 1,000 |
| 4. Balance Inquiry | NA | 400 |
| 5. Mini Statement | NA | 400 |
| 6. Popote ATM card issuance /Replacement | N/A | 15,000 |
| 7. Annual Card maintainance | N/A | 10,000 |
| 8. PIN Re-issue | N/A | 1,000 |
| 9. Collection of ATM card at non-domicileBranch | N/A | 6,500 |
| 10. Uncollected and Destroyed ATM Card | N/A | N/A |
| 11. Card Maintainance | N/A | 5,000 |
| 12. Failed Transaction Due to insufficient fund | | 900 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

## GUARANTEE

| | CHARGES |
|---|---|
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

## POPOTE VISA CARD


| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote VISA issuance/Replacement | 15,000.00 |
| Annual Card Maintainance | 10,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,350.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 5,500.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

**TABASAMU ACCOUNT**

- Ni akaunti kwa Wanawake (mmoja mmoja au Kikundi)
- Haina gharama za Uendeshaji
- Inalenga kuboresha maisha ya Mwanamke

Mwanamke wa Nguvu, Pambana Kiuchumi



Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683 Namba bila Malipo: 0800110160

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wazazi wana jukumu kubwa kudhibiti mmomonyoko huu

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan wakati akizungumza katika maadhimisho ya mwaka mpya wa Kiislamu, alitoa tahadhari kuhusu mmomonyoko wa maadili ambao unalikumba taifa hivi sasa.

Mmomonyoko huo wa maadili umekuwa ni kilio katika kila sehemu, iwe shuleni, nyumbani, sehemu ya kazi na zingine ambazo mtu hawezi kudhani kuwa kunaweza kukatokea hali hiyo.

Kilio hicho sasa kimekuwa kikisikika kutoka kwa viongozi wa dini na viongozi wa kitaifa wakikemea ili vitokomee nchini.

Tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa kiasi kikubwa linaanzia nyumbani ambako mtoto hupata msingi wa malezi bora.

Kama mtoto hakujengwa kwenye msingi wa malezi bora maisha yake hayatakuwa mazuri kwa sababu atakuwa amekosa mwelekeo.

Hata watu wanaosababisha kuwapo kwa mmomonyoko huo nao pia hawakupata misingi mizuri ya maisha.

Ndiyo maana wanasaikolojia wanashauri kuwa mtoto tangu anapokuwa tumboni mwa mwa mama yake anatakiwa kusemewa maneno mazuri ili hata anapozaliwa anakuwa amejengeka.

Wanasaikolojia wanasema kama mama anapokuwa mjamzito akipenda kusoma vitabu, basi hata mtoto atakapozaliwa atakuwa na akili.

Wakati wa enzi za mabibi na mababu, watoto katika jamii walikuwa wakilelewa na mtu yeyote akikanywa anasikia.

Wazee walikuwa wakimkuta mtoto ambaye siyo wa kumzaa yeye anafanya jambo ambalo si la kimaadili atamkanya pale pale na kumpeleka hadi kwa mzazi wake na kumweleza alichokuwa akifanya mtoto na mzazi naye hulipokea kwa mtazamo chanya.

Lakini, siku hizi maadili yameporomoka kiasi kwamba mtu akitokea kumkanya mtoto ambaye siyo wa kwake na akaenda kumweleza mzazi, basi huyo mzazi atatoka na kanga mkononi kwenda kumshambulia mtu aliyemkanya mwanawe.

Hilo pia linatokea shuleni, iwapo mwalimu atamwadhibu mtoto kwa kufanya jambo baya na mtoto huyo akienda kumweleza mzazi, atakwenda kumfokea huyo mwalimu na kumuonya aache kumwadhibu mwanawe.

Katika hali kama hii ni lazima maadili yataporomoka kwa sababu mtoto anajua anaweza kufanya jambo lolote na hakuna mtu mwingine atakayethubutu kumwadhibu.

Na katika hili la mmomonyoko wa maadili imeshashuhudiwa watoto wakipigana na watu wazima au walimu wao wanapojaribu kuwaonya.

Wazazi wengine wamejitoa kabisa katika malezi ya watoto wao na kuwapeleka kwa bibi zao wakawalee na wakati mwingine wazee hao wanakuwa wamekula chumvi nyingi kiasi cha kushindwa kuwaonya wajukuu zao.

Pia, baadhi ya wazazi huwa ndiyo chanzo cha watoto wao kuwa na mmomonyoko wa maadili kutokana na vitendo wanavyofanya mbele yao.

Watoto hawafuatiliwi wanacheza na nani na hata muda wa kurudi nyumbani hawaulizwi. Matokeo yake wanajilea wenyewe na kufuata matendo yanayowafanywa mitaani kwa sababu hakuna mtu wa kuwaongoza.

Rais Samia juzi amesema kuwa mmomonyoko wa maadili nchini ni ugonjwa unaoliandamama taifa na jamii inaathrika na ukatili wa kijinsia. Wizi na matumizi ya dawa za kulevya ni mambo yanayolitia aibu taifa na familia kwa ujumla.

Mpaka Rais analizungumza hili, tatizo limefika mahali pabaya hivyo nguvu ya ziada inahitajika kulitatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko: Dennis Ntaita,** 0713 578284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Sayansi ya kompyuta iibue wabunifu

**SAYANSI** ya kompyuta ni moja ya mapendekezo ya Wizara ya Elimu katika mchakato wa mabadiliko ya sera mpya ya elimu, mafunzo na mitaala ambayo imo kwenye rasimu iliojadiliwa na kupitiwa na wadau wa elimu hivi karibuni.

Matumizi ya kompyuta, hasa zile ambazo zimeunganishwa na mtandao wa intaneti katika sekta ya elimu, ni moja ya njia zinazotajwa kuwa zinaweza kusaidia kuboresha hali ya utoaji elimu shuleni.

Hiyo inatokana na kwamba, mwanafunzi kutumia intaneti anaweza kupata maarifa makubwa ambayo yanaweza kumsaidia katika maisha yake ya baadaye, hasa katika nchi kama hii ambayo ina uhaba mkubwa wa walimu. Kutokana na umuhimu huo wa matumizi ya kompyuta, sasa somo la sayansi ya kompyuta ni moja ya mapendekezo ya Wizara ya Elimu katika mchakato wa mabadiliko ya Sera, Mafunzo na ile ya Mitaala ambayo imo kwenye rasimu iliokuwa ikijadiliwa na kupitiwa na wadau wa elimu hivi karibuni.

Lengo la serikali katika mabadiliko ya sera mpya ya elimu, mafunzo na mitaala, kutakuwa na somo jipya la sayansi ya kompyuta, kwa kuwa kuwapo kwa somo hilo, ni kutaka kusaidia wanafunzi kuwa wataalamu wabunifu na wadadisi kwenye eneo hilo.

Vilevile si kuishia hapo tu bali hatua hiyo inalenga kuwawezesha wanafunzi kuwa na ujuzi wa kuzitengeneza na hivyo kukuza ujuzi huo kwenye katika TEHAMA na hata kuweza kuwa wabunifu zaidi.

Binafsi ninaamini kuwa somo hilo limekuja kwa wakati wake hasa kwa kuzingatia kwamba kwa sasa dunia imekuwa kama kijiji, kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Jambo la muhimu hapa ni kutafuta jinsi ya kuwapa walimu mafunzo yenye mbinu mpya za matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Kama ambavyo mafunzo yamekuwa yalifanyika kwa walimu, ili kuelewa matumizi sahihi ya vishikwambi, ni vyema yakaendelea kuimarishwa zaidi, ili nao wakamudu vyema kufundisha somo la sayansi ya kompyuta.

Mabadiliko mtaala wa elimu kuja na somo jipya la sayansi ya kompyuta, ninadhani ni hatua nzuri zilizochukuliwa na wizara hasa kwa kutambua kuwa dunia inakwenda kwa kasi kwenye masuala ya sayansi na teknolojia.

Kwa kuwa serikali ina mikakati ya kuhakikisha elimu inatolewa kwa njia ya TEHAMA, ninadhani ni vyema kutoa mafunzo kwenye vyuo vyote vya ualimu, ili kuwawezesha walimu watarajiwa kuwa na elimu ya teknolojia hiyo.

Walimu hao na wengine waliopo kazini wakipata elimu ya matumizi ya kompyuta, itawawezesha kufundisha kwa urahisi na kwa ufasaha shuleni, na hivyo kupanua wigo wa sayansi na teknolojia.

Hadi sasa inaelezwa kuwa wanafunzi wanaosomea ualimu kwenye vyuo vyote vya serikali, wanafundishwa jinsi ya kutumia TEHAMA kufundisha, ikiwa ni mkakati mojawapo wa kuhakikisha wanaweza kutoa elimu kwa njia hiyo.

Si hao ni bali pia walimu waliopo vyuoni na waliopo shuleni hasa wale wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza nao wanafundishwa jinsi ya kutumia teknolojia hiyo kuwafundisha wanafunzi wao.

Kimsingi, ufundishaji shuleni kwa njia ya TEHAMA unawezekana na utasaidia nchi kwenda wakati, lakini ninadhani bado kuna kikwazo ambacho kinatakiwa kuondolewa haraka kadri inavyowezekana.

Kikwazo hicho ni ukosefu wa miundombinu ya umeme kwenye baadhi ya shule, hali ambayo si rahisi kufundisha somo la sayansi ya kompyuta kama hakuna nishati hiyo muhimu shuleni.

Ninaamini hakuna lisilowezekana chini ya jua, hivyo ingependeza kama kila shule kuanzia mijini hadi vijijini, itakuwa na miundombinu ya umeme, kwani kufundisha kwa TEHAMA kunawezekana.

Kupitia TEHAMA mwanafunzi inaweza kupata maarifa mbalimbali na hata ujuzi wa kumwezesha kuwa mbunifu, hivyo ni wakati sasa wa kuhakikisha lengo la kuwa na somo la sayansi ya kompyuta linatimia.

Lakini pia uwapo wa somo la sayansi ya kompyuta, utaifanya Tanzania kuungana na baadhi ya nchi jirani ambazo kwa muda mrefu wanafunzi wake wamekuwa wakitumia kompyuta shuleni.

# Watanzania 20 wafanyiwa upasuaji moyo tundu dogo

**Na Joseph Mwendapole**

WAGONJWA 20 wenye matatizo ya mfumo wa umeme wa moyo wamefanyiwa upasuaji wa tundu dogo kwa kutumia mtambo wa Cathlab katika kambi maalum iliyofanywa na wataalamu wa afya wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Wataalamu hao walishirikiana na wenzao kutoka Shirika la Madaktari Afrika la nchini Marekani.

Kambi hiyo ya siku tano iliyomalizika mwishoni mwa wiki ililenga kuwahudumia wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa umeme wa moyo, kuwasaidia wataalamu wa afya ambao wapo masomoni kujifunza zaidi na kuongeza wigo wa wataalamu wa afya.

Akizungumzia kambi hiyo, Daktari bingwa wa magonjwa ya moyo na mfumo wa umeme wa moyo wa JKCI, Yona Gandye, alisema wagonjwa hao 20 waliofanyiwa upasuaji katika kambi hiyo walipaswa kulipa siyo chini ya Sh. milioni 500, lakini kupitia wenzao wa Shirika la Madaktari Afrika, baadhi ya wagonjwa wamepata msamaha na kuwaondolea gharama za matibabu yao.

“Wagonjwa tuliowafanyia upasuaji wapo ambao mapigo yao ya moyo yalikuwa yakienda chini sana (heart block) na wengine mapigo yao ya moyo yalikuwa yanaenda haraka sana,” alisema Dk. Gandye.

Dk. Gandye alisema magonjwa yanayohusisha mfumo wa umeme wa moyo mara nyingi huwa na sababu mbalimbali zinazosababisha hitilafu ya utengenezaji wa mapigo ya moyo ikiwamo kuzaliwa na tatizo hilo ama kupata kutokana na kuwa na magonjwa mengine kama shinikizo la juu la damu, moyo kutanuka na kuwa na shambulio la moyo (heart attack).

“Mgonjwa anapopata tatizo la mapigo ya moyo kwenda juu au kuwa chini anakuwa katika hali ya hatari hivyo anaweza kufariki ghafla ama kuusababishia moyo kushindwa kufanya kazi,” alisema Dk. Gandye.

Daktari kutoka Shirika la Madaktari Afrika la nchini Marekani, Nitish Badhwar, alisema JKCI ni moja ya hospitali iliyowekezwa vifaa vya kisasa vya kuhudumia wagonjwa wa moyo na kutoka Tanzania waitumie hospitali hiyo vizuri kwa kuwa hakuna haja kufuata huduma za matibabu ya moyo nje ya nchi.

Dk. Nitish alisema kutokana na vifaa vya matibabu ya moyo kuwa na gharama kubwa Shirika la Madaktari Afrika liliamua kutuma vifaa ili kuwasaidia wagonjwa ambao hawana uwezo wa kugharamia matibabu ikiwa ni sehemu ya kutoa shukrani kwa jamii pamoja na kuokoa maisha.

“Hii ni mara yangu ya kwanza kufika Tanzania, nimefurahishwa na huduma zinazotolewa katika Taasisi hii, katika kambi hii nimepata nafasi ya kubadilishana ujuzi na madaktari wa JKCI na kuoana ni kwa kiasi gani wameendelea kwani sasa wagonjwa wa moyo Watanzania hawana haja ya kutafuta matibabu nje ya nchi,” alisema Dk. Nitish.

Mgonjwa aliyefanyiwa upasuaji katika kambi hiyo kutoka mkoani Dodoma, Jafari Musa, alisema gharama za matibabu yake zilifika Sh. milioni 18, lakini kutokana na hali yake ya maisha kutokumudu kiasi hicho cha fedha uongozi wa taasisi uliruhusu apatiwe matibabu bila gharama.

“Naishukuru Serikali ya Tanzania, Uongozi wa JKCI pamoja na madaktari kutoka Marekani kwa kunipatia msamaha wa matibabu kwani sasa najisikia vizuri baada ya kukaa ndani ya chumba cha upasuaji zaidi ya masaa manne madaktari wakitumia utaalamu wao kuokoa maisha yangu,” alisema Jafari.

Aidha, Jafari aliwataka Watanzania kuwa na imani na taasisi hiyo ambayo inatoa huduma bora kwa wagonjwa wa moyo, wataalamu wake huwa karibu na wagonjwa wakati wote kufuatilia hali za wagonjwa mara kwa mara.

## EAC yaombwa kuingilia sakata la Kenya

**Na Maulid Mmbaga**

WAKUU wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wameombwa kuingilia kati sakata linaloendelea nchini Kenya kati ya serikali na kiongozi wa upinzani, baada ya kuendelea kushuhudiwa sintofahamu inayohatarisha usalama wa wananchi na kugharimu maisha yao.

Akizungumza jana mkoani Pwani, mfanyabiashara mashuhuri na kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mohamed Abood mkazi wa Bagamoyo, alisema mvutano unaoendelea Kenya una ishara zote hatarishi za kuishi kwa machafuko na watu wasio na hatia kujikuta wakipoteza maisha. Kenya kumekuwa kukishuhudiwa vurugu zinazotajwa kusababishwa na maandamano ya kuipinga serikali yanayodaiwa kuratibiwa na kiongozi wa kambi ya upinzani Azimio la Umoja, Raila Odinga.

Kutokana na hali hiyo Rais wa Kenya, William Ruto, siku chache zilizopita akizungumza katika mji wa Mai Mahiu kaunti ya Nakuru, alinukuliwa akimshutumu mtangulizi wake mstaafu Uhuru Kenyatta kwa madai ya kushirikiana na Odinga anayetajwa kuitisha maandamano yanayosababisha uvunjifu wa amani nchini humo.

Pia, Rais Ruto alimtahadharisha Odinga kuendelea na maandamano yake yaliyopangwa kufanyika wiki hii, akisema serikali itamchukulia hatua kali iwapo umwagaji damu zaidi utashuhudiwa katika mchakato huo.

Alisema kwa kuwa Kenya ni mwanachama wa EAC ipo haja kwa wakuu wa nchi au marais wastaafu wa kanda ya Afrika Mashariki kujitokeza na kutafuta namna ya kuumaliza mvutano unaoendelea.

“Endapo watajiweka kando na kufanya kama hawaoni kinachotokea Kenya, siku moja watalazimika kwenda nchini humo ili kuzikutanisha pande mbili za utawala na upinzani wakati huo kukiwa na hali mbaya,” alitahadharisha na kuongeza;

Alisema endapo hatari na machafuko yoyote yatazidi kuchomoza Kenya, nchi zote jirani hawatakwepa kubeba matatizo au gharama ya mzozo huo.


ACB
AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
benki kwa maendeleo yako



Buriani Mzee Rashidi Mbuguni
1952-2023

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Akiba Commercial Bank Plc wamepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Bw. Rashid Mbuguni, aliyekuwa mmoja wa waasisi wa benki hii.

Marehemu Mbuguni alikuwa na mchango mkubwa katika kuanzishwa kwa benki ya Akiba, tangu kuzaliwa kwa wazo la kuanzishwa kwa Benki pamoja na mchakato mzima wa kufanikisha ufunguzi rasmi wa taasisi.

Aidha, alitoa mchango mkubwa kwa kuhudumu kwenye Bodi kwa muda mrefu kuanzia 1997 hadi 2008.

Uongozi wake, maono na moyo wa kuitumikia taasisi hii katika kipindi cha uhai wake vimeacha alama ambayo haitafutika. Yale yote aliyoyafanya yataendelea kuwa taa inayotuongoza tunapoendelea kudumisha misingi iliyoiweka kwenye taasisi yetu kama sehemu ya kumuenzi.

Inalillaahi Wainna Ilaihi Raajiuun

Akiba Commercial Bank Plc



217502402

+255 (746) 811510
support@acbtz.com | www.acbbank.co.tz
OPEN DOOR OF POSSIBILITIES and MORE




Kaimu Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Maud Droogleever Fortuyn, akitoa salamu za shirika hilo, katika warsha ya viongozi wa dini kuhusu wajibu wa wazazi na walezi, katika malezi na familia Tanzania, ambayo iliandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wanawake na Makundi Maalum na kufanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TIC yavunja rekodi kusajili zaidi miradi 200 miezi 6

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji nchini (TIC), kimevunja rekodi kwa kufanikiwa kusajili miradi 229 kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, huku ikitarajia kusajili miradi 450 mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Kituo hicho, Gilead Teri, wakati akizungumza kwenye mkutano na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam.

Alisema kwa mwaka 2021 TIC ilifanikiwa kusajili miradi 256 na mwaka 2022 miradi 293 hivyo kusajili miradi 229 kwa nusu ya mwaka huu.

Alisema mpaka sasa miradi iliyokwishasajiliwa kwa mwaka huu ina thamani ya Dola za Marekani bilioni 2.2 ambazo ni sawa na Sh. trilioni 4.5.

"Ukijumlisha hizi fedha na za mwaka jana ambazo ni Dola bilioni 4.5 unapata karibu trilioni 10, ukijumlisha na za mwaka 2021 tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani tunapata jumla ya Dola za Marekani bilioni 10 ambazo ni sawa na Sh. trilioni 22 katika uwekezaji wa miaka miwili tu," alisema.

Alisema kupata uwekezaji wa thamani kubwa kiasi hicho ndani ya muda mfupi ni mafanikio makubwa na ya kujivunia kwani kwenye miaka sita ya awamu ya tano kiwango cha uwekezaji kilishuka sana kulinganisha na hali ilivyo kwa sasa.

Teri alisema Rais Samia ameelekeza nguvu kwenye kuweka sheria rafiki kwa wawekezaji pamoja na vivutio vya aina mbalimbali ambavyo vimewafanya wawekezaji kuja kwa wingi.

Alisema TIC imejitahidi kuendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kuhakikisha huduma nyingi zinapatikana kwa pamoja na kuondoa usumbufu wa awali ambao wawekezaji walikuwa wakiupata.

Alisema hata vibali vya kazi vimekuwa vikitolewa kwa urahisi kwa mwekezaji ambaye nyaraka zake zimekamilika kulinganisha na muda ambao ulikuwa ukitumika miaka ya nyuma hali ambayo alisema iliwakatisha tamaa wawekezaji.

Mkurugenzi huyo alisema TIC imeweka mikakati mbalimbali kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vya sukari na kwamba hadi mwishoni mwa mwaka ujao Tanzania itakuwa inajitosheleza kwa sukari ya nyumbani.

Alisema kiwanda cha sukari cha ubia cha Mkulazi nacho kinaendelea vizuri na kinatarajia kuanza uzalishaji wa sukari hivi karibuni ambapo kitapunguza utegemezi wa sukari ya kuagiza nje ya nchi wakati mwingine huleta shida miongoni mwa wafanyabiashara.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa kongani za biashara maeneo ya Kibaha Mkoa wa Pwani na moja ya kongani hizo itakuwa na viwanda zaidi ya 203.

Alisema TIC inaendelea kuzungumza na wawekezaji mbalimbali na kuwapa vivutio ili waje kuwekeza nchini kwenye utengenezaji wa vifaa vya elektroniki kama simu, kamera na vifaa vingine vya aina hiyo.

Aliwataka Watanzania wanaotaka kuwekezaji kwenye viwanda kwenda kujisajili TIC ili wapate vyeti vitakavyowasaidia kupata nafuu ya ushuru wa bidhaa za mitaji kama wanavyopata wawekezaji wa kigeni.

"Ili kusajiliwa TIC mwekezaji mzalendo anapaswa kuwa na mtaji wa Dola za Marekani 50,000 tu na siyo lazima awe na fedha taslimu badala yake mtaji huo unaweza kukawa thamani ya mitambo aliyonayo, ardhi, magari aliyonayo. Kwa hiyo akisajili TIC anapata unafuu wa ushuru wa kulinda bidhaa mtaji anazoingiza," alisema.

## UN kumuenzi Mandela kuwapa msaada wagonjwa wa saratani

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIKA kumuenzi Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, Umoja wa Mataifa (UN) na Ubalozi wa Afrika Kusini wanatarajia kutoa msaada kwa watoto wanaougua ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Balozi wa Afrika Kusini nchini Tanzania, Noluthando Mayende-Malepe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kumbukizi ya kifo cha Nelson Mandela, maadhimisho yatakayofanyika kwa siku tatu kuanzia Julai 18 hadi 20.

Alisema katika kumbukizi hiyo UN na Ubalozi wa Afrika Kusini watatembelea idara ya saratani ya watoto MNH, lengo likiwa ni kuongeza uelewa kuhusu matatizo yanayowakabili watoto wanaougua saratani na kuweka msisitizo juu ya umuhimu wa upatikanaji wa huduma bora za afya.

"Watoto walikuwa na nafasi maalum sana katika moyo wa Nelson Mandela. Hivyo napata faraja kubwa kwa mwaka huu tutashirikiana na UN Tanzania katika kusaidia watoto wanaopambana na saratani," alisema.

Alisema pia katika maadhimisho hayo, kutakuwapo na mjadala wa kutoa elimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), utakaoongozwa na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete.

Alisema Kikwete atatoa hotuba muhimu kuhusu kumbukumbu ya Nelson Mandela, miaka 10 ya kifo chake.

Naye Mkuu wa Ofisi ya Mratibu Mkaazi wa mashirika ya UN Tanzania, Shabnam Mallick, alisema katika kumbukizi ya kifo cha Nelson Mandela watashiriki kikamirifu kwa sababu kiongozi huyo alikuwa na mchango mkubwa katika harataki za kudai uhuru pamoja na kupigania haki.

Alisema: "Ushirikiano huu unathibitisha dhamira yetu ya pamoja kusimama na haki za binadamu, maendeleo endelevu, kukuza jamii yenye ushirikiano zaidi na kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayeachwa nyuma."

Alisema UN inalengo la kufanya mabadiliko ya kweli katika maisha ya watoto walio hatarini na kuhamasisha kizazi kijacho kuendeleza mambo mazuri yaliyofanywa na Nelson Mandela.

# Wadau wa Songwe wafunguka uwekezaji bandari

**Na Moses Ng'wat**, TUNDUMA

VIONGOZI wa Serikali ya Wilaya ya Momba na Halmashauri ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe, wamejitosa kwenye sakata la bandari kwa kueleza kuwa wanaopinga uwekezaji huo wamekuwa wakinufaika na mambo yasiyo na tija yaliyokuwa yakifanyika bandarini.

Viongozi hao ambao ni Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fakh Lulandala, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Frank Nkinda na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Philemon Magesa, walizungumza na waandishi wa habari kuhusu uwekezaji bandarini unaotarajiwa kufanywa na Kampuni ya DP World.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Lulandala akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema, wameamua kuzungumzia suala hilo kwasababu wilaya hiyo hususani Halmashauri ya Mji wa Tunduma imekuwa mnufaika mkubwa wa mizigo inayotoka Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kwa siku halmashauri hiyo imekuwa ikikusanya ushuru kati ya Shilingi milioni nane hadi 10 kutokana na maegesho ya malori yanayosafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda nje kupitia mpaka wa Tunduma hivyo iwapo uwekezaji zaidi utafanyika katika bandari hiyo na mizigo kuongezeka mapato yataongezeka maradufu.

Lulandala alisema sisi kama Watanzania tunahitaji mwekezaji ambaye ataendesha bandari kwa ufanisi na kuongeza mapato na kwamba mfano katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma kuna zaidi ya ekari 2,000 zilizotengwa kwa ajili ya watu wanaotaka kuwekeza hivyo hata kampuni ya DP World kama atapewa atakaribishwa Tunduma kwa ajili kuwekeza bandari kavu (Dry Port).

Aidha, alisema, mkataba unaandaliwa na watu, inawezekana kuwapo upungufu maeneo ambayo hayajakaa sawa ndiyo maana suala hili lilipelekwa bungeni kufanyiwa marekebisho na kwamba wasomi na wanasheria wasijifanye kuwa wanajua kuliko wabunge na kila anayeunga mkono wanaona kapewa rushwa na anayepinga kwanini tusione naye kapewa rushwa.

"Mkataba wa DP World sisi kwetu Tunduma ukifanyika utawezesha wawekezaji waje wafunge mitambo mikubwa yenye uwezo zaidi ya kufanya kazi kwa kiwango ambacho kitaongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam na hivyo kuvutia wafanyabiashara kote duniani kupitishia mizigo yao katika bandari hiyo," alisema.

Lulandala alisema pia DP World watafunga mifumo ya kisasa ambayo itakuwa ikisomana na mifumo ya serikali na taasisi nyingine kama Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hivyo mizigo itakayokuwa inaingia na kutoka itajulikana kwa hesabu zake hakutakuwa na kuficha mfukoni.

Alisema kuna hoja inayoelezwa na wanaopinga uwekezaji huo kwamba Bandari ya Dar es Salaam imeuzwa, lakini wakiulizwa imeuzwa shilingi ngapi na kama imeuzwa maana yake TPA haitaendelea, lakini wanakosa majibu.



# Raia wa Ethiopia wakamatwa wakiingia nchini kinyemela

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

RAIA 12 wa Ethiopia, wamekamatwa katika eneo la Mtuka, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, kwa tuhuma za kuingia nchini bila kibali na kusafiri kwa kificho kuelekea mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Baada ya kufikia mikoa hiyo ikiwamo Mbeya, hukimbilia mpakani kupitia njia za panya kwenda nchini Afrika Kusini kutafuta kazi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, wahamiaji hao walikuwa wakisafirishwa kwa kutumia gari dogo, aina ya Mark X yenye namba za usajili T 215 DDY ikitokea Mkoa wa Arusha.

Wahamiaji hao walikamatwa juzi, majira ya saa 5:00 asubuhi katika Kijiji cha Chemchem kilichoko Kata ya Mtuka.

Kamanda Katabazi, aliwataja waliokamatwa kuwa ni Kliiu Tekel (18), Chrente Alumu (17), Baraka Gadafa (17), Samweli Yemeke (17), Algeze Arenga(17), Maratu Wotso (18) na Buruk Charine (18). "Tulipopata taarifa tuliweka mtego wa kuikamata hii gari, hata hivyo dereva wa gari hilo baada ya kugundua kuwa anafuatiliwa alichepuka toka barabara kuu na kuingia barabara ya changarawe kwenda Kijiji cha Chemchem, ndio tuliwakamatia," alisema Katabazi.

Aidha, alisema upelelezi bado unaendelea ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi, limetangaza kumsaka dereva wa gari yenye namba za usajili T.465 aina ya Toyota Noah, ambaye hakufahamika majina kutokana na tuhuma za kusafiafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi.

Gari hilo lilikutwa limebeba bunda 264 za mirungi, sawa na kilogramu 110.

Katabazi, alisema mirungi hiyo ilikuwa inasafirishwa kwenda Babati kutoka Arusha ila waliweka mtego dereva alipougundua alisimama na kukimbia kusikojulikana.

# Wakazi Kijiji Nakweni wajengewa zahanati

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAKAZI wa Kijiji cha Nakweni, Kata ya Shambarai Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, waliokuwa wanatembea kilometa 12 kwenda Mirerani kufuata huduma za afya, wameondokana na adha hiyo, baada ya Taasisi ya All for His Glory kuwajengewa zahanati.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Askofu wa Kanisa la International Evangelisim, Dk.Israel Ole Maasa, alisema wameguswa kuwajengea wananchi hao zahanati kutokana na gharama kubwa wanazoingia kusafiri kila siku kufuata huduma za tiba nje ya Kijiji chao.

Alisema, pia wamechimba visima virefu vitatu kwa ajili ya wakazi wa kijiji hicho chenye wakazi 8,952, ambao ni wafugaji na wakulima.

Naibu Waziri wa Afya, Dk.Godwin Mollel, akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya zahanati hiyo, aliishukuru taasisi hiyo ya dini kwa kufanikisha ujenzi wa mradi huo.

"Baba Askofu, Dk. Israel Ole Maasa, nawashukuru mno kwa niaba ya serikali kwa kufanikisha ujenzi wa zahanati hii, itakayokuwa msaada mkubwa kwa jamii ya eneo hili," alisema Dk. Mollel.

Aliwashukuru wakazi wa kijiji hicho, kwa kuwapokea vizuri kwa kuwatandikia kanga barabarani ili wapite juu kuonesha furaha ya kupokea zahanati hiyo.

Kabla ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alisema watumishi wawili, daktari na muuguzi, tayari wameandaliwa kuanza kazi jengo hilo likikamilika.

"Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Simanjiro (DMO), Dk. Aristidy Raphael, ambaye najivunia uchapakazi wake, tayari ameshawaandaa watumishi wawili kuanza kazi kwenye hii zahanati," alisema Dk. Serera.

Awali, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Noel Mollel, alisema nguvu za wananchi zimetumika kwenye ujenzi wa vyumba vinane hadi kufikia kwenye lenta na kugharimu Sh. milioni 10.

Mkazi wa kijiji hicho, Naishok Zephania, alisema kumekuwapo na tatizo la wagonjwa hasa kwa wajawazito kwenda kufuata huduma za afya umbali mrefu, lakini kutokana na ujenzi huo, tatizo limefika ukingoni zahanati hiyo ikianza kazi.


# NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED, AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED na HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DAMAS JOACHIM KADULA | CONCEPTER HERMES KADULA | NYUMBA (PARCEL NO. TMK/AZM/KGN33/6 TMK040533) | KICHANGANI, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 01/08/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 2 | PATRICK P. NDARO | PATRICK P. NDARO | NYUMBA | KIVULE, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 04/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 3 | MUSA IDDI MAKENYA | MUSA IDDI MAKENYA | NYUMBA | MWEMBE BAMIA, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 04/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 4 | KAISER ALLOYCE KINYANGA | KAISER ALLOYCE KINYANGASI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MTAA WA MBWATE, KATA YA MKUZA , WILAYA YA KIBAHA, PWANI | 31/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 5 | JANE J. MOSHA | VICENT SILVESTA KESSY | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MTAA WA MSUFINI, CHAMANZI, KATA YA KIBONDE MAJI WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 31/07/2023 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 6 | REHEMA PETER KISSILA | REHEMA PETER KISSILA | NYUMBA | KIJIJI CHA KISERIANI, KATA YA MLANGARINI, ARUSHA | 03/08/2023 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT |
| 7 | GAIMO CONSTRUCTION COMPANY LIMITED | GAUDENCE VICENT LYIMO AND MONICA GAUDENCE LYIMO | NYUMBA YENYE HATI YA MAKAZI No.21393, PLOT No.407, BLOCK 'JJ' | OLOIRIEN, MANISPAA YA ARUSHA, ARUSHA | 07/08/2023 SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT |


**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | | |
|---|---|---|
| **TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**<br>**P.O. Box 1305**<br>**Songea, Ruvuma**<br>**Tel: 0716070298, 0754881926, 0784718734**<br>**Email: twinscoltd5@gmail.com** | **AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED**<br>**P. O. Box 62163**<br>**Dar es Salaam**<br>**Tel: 0658100737, 0757276263**<br>**Email: amazauctionma@gmail.com** | **HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**<br>**P.o.Box 11898**<br>**Arusha**<br>**Tel: 0784 200283/ 0767529605**<br>**Email: harvestercapital558@gmail.com** |

217502302



HABARI KANDA YA ZIWA

# Zaidi ya miti milioni moja yapandwa kwa mwaka

**Na Vitus Audax,**
SENGEREMA

ZAIDI ya miti milioni 1.5 imependwa katika Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza kwa kipindi cha mwaka 2022/23 kwa lengo la kuhifadhi na kutunza mazingira hali iliyoonesha kumfurahisha kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa.

Akitoa taarifa kwa kiongozi wa mbio za Mwenge kuhusu utekelezaji wa mradi huo uliopo chini ya usimamizi wa TFS wilaya, Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Walter Njau, alisema halmashauri hiyo imejikita kutunza vyanzo vya maji, kurejesha uoto wa asili na ikolojia ya viumbe hai na utunzaji wa mazingira kwa kupata miti ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda, miti ya mbao na ya asili.

Alisema miti iliyopandwa kwa kipindi cha mwaka 2022/23 ni 1,513,700 na kueleza kuwa bado wanaendelea na upandaji miti kwa kuangalia maeneo yenye uhitaji zaidi ikiwa ni pamoja na maeneo ya taasisi na vyanzo vya maji.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge 2023, Abdalla Shaibu Kaim, alipongeza halmashauri pamoja na viongozi wake kwa kuweka juhudi katika kutunza na kuhifadhi mazingira huku akiwataka kuendeleza juhudi za kuitunza.

"Katika uhifadhi mmeibuka mabingwa na hili ndilo takwa la serikali na ulimwengu kwa ujumla hongereni sana, lakini jitahidi sana kuitunza maana itakuja kuwalipeni ninyi na taifa kwa ujumla," alisema kiongozi huyo.

"Kaulimbiu ya mbio za Mwenge kwa mwaka huu ni 'Tunza mazingira, okoa vyanzo vya maji kwa ustawi wa viumbe hai kwa uchumi wa Taifa' endeleeni kulisimamia hili."

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga alisema, katika kuhakikisha wanakijanisha wilaya hiyo kwa ujumla wameendelea kushirikiana vyema na wadau wa mazingira kupanda miti kwa wingi na kuiwekea ulinzi kwa kushirikiana na jamii inayozizunguka.

# RC aagiza ukaguzi mara kwa mara bwawa la mgodi

**Na Marco Maduhu,**
KICHAPU



MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (pichani), ameagiza Mgodi wa Almasi Mwadui, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika bwawa jipya la Majitope ili lisiweze kubomoka na kuleta madhara kwa wananchi.

Mndeme alibainisha hayo jana wakati akizindua rasmi uzalishaji wa madini ya almasi katika Mgodi wa Mwadui, baada ya kusimama kwa muda wa miezi minane kutokana na bwawa la awali la Majitope kupasuka.

Alisema amefarijika kuona mgodi huo una anza tena shughuli za uzalishaji madini, baada ya ujenzi wa bwawa jipya la kuhifadhia Majitope kukamilika, jambo ambalo serikali itapata mapato pamoja na wananchi kutekelezewa miradi ya maendeleo kupitia CSR.

"Sasa hakikisha mnafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika bwawa hili jipya hili kusije kutokea kama bwawa la awali na kuleta madhara kwa wananchi, kadhalika hakikisheni mnaanza usanifu wa kujenga bwawa jingine jipya ili hili likijaa msisimamishe tena uzalishaji," alisema Mndeme.

Aliagiza uongozi huo wa mgodi kuongeza pia kasi ya uzalishaji wa madini, na kufidia muda ambao wameupoteza kwa kipindi walichosimamisha uzalishaji.

Naye Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Mhandisi Ayoub Mwenda, alisema bwawa hilo jipya ni la kipindi cha miaka miwili linajaa na hivi karibuni wataanza usanifu wa bwawa jingine jipya ambalo litakuwa la kipindi kirefu.

Alisema kwa muda muda huo ambao wamesimamisha uzalishaji wa madini wamepoteza fedha nyingi, kwa mwezi mmoja walikuwa wakizalisha madini karati 25 hadi 30 na moja inauzwa kwa Dola za Marekani 270.

Mhandisi Mwelekezi kutoka Kampuni ya City Enginering, Aniel Macha, ndiyo walikuwa wakijenga bwawa hilo jipya, alisema wamelijenga kwa ubora wa hali ya juu na halitaweza kuleta madhara tena kwa wananchi.

Alisema wameweka vipimo, vitakavyokuwa vikionyesha kama kuna shida mahali na kisha kuifuatilia na kufanya matengenezo ili lisije kupasuka na kuleta madhara kwa wananchi kama bwawa la awali.

Alisema pia kila baada ya miezi mitatu watakuwa wakilifanyia ukaguzi kuhakikisha usalama wake na kuwatoa wasiwasi wananchi kuwa hawataweza kupata madhara tena.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

### UNAUDITED RESULTS FOR THE SIX MONTHS ENDED 30 JUNE 2023

CHAIRMAN'S STATEMENT

Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong operating results when compared to the same period in year 2022. The Company has experienced a rather stable growth of sales volume and revenue compared to the same period in 2022. During this period revenue increased by 8%.

This increase is mainly due to the process improvement and cost control in our production. Plant availability and efficiency played a vital role to the improved performance in the first half of year 2023. On top of the operational excellence, the Company continued to improve in the area of Health and Safety, with ZERO loss of time to injury (LTI) recorded in 2023.

The Company continues to focus on customer service, selling new products within our high quality portfolio. We maintain strong customer relationships to enable TPCPLC to demonstrate its strength as the leading player in the industry.

Prospects
In spite of the cement demand growing slowly this year, we are optimistic about the second half of the year. TPCPLC will continue to work on improving efficiency and operating performance.

Appreciation
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board

STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2023

| TZS '000 | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 246,284,758 | 227,512,642 |
| Cost of sales | (166,235,904) | (149,714,492) |
| **Gross profit** | **80,048,854** | **77,798,150** |
| | | |
| Other operating income | 1,620,524 | 757,134 |
| Selling and marketing expenses | (1,468,800) | (1,413,469) |
| Administrative expenses | (12,026,402) | (10,468,251) |
| Other operating expenses | (1,294,037) | (1,502,923) |
| **Operating profit** | **66,880,139** | **65,170,641** |
| | | |
| Finance income | 1,481,873 | 1,710,838 |
| Finance costs | (308,890) | (639,468) |
| Net gain on foreign currency translation | 3,976,167 | 1,059,686 |
| **Profit before tax** | **72,029,289** | **65,301,697** |
| | | |
| Income tax expense | (22,026,418) | 20,248,978) |
| **Profit for the year** | **50,002,871** | **47,052,719** |

STATEMENT OF FINANCIAL POSITION
AS AT 30 JUNE 2023

| TZS '000 | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Non-current assets** | | |
| Property, plant and equipment | 136,081,672 | 140,402,982 |
| Intangible assets | 797,217 | 909,928 |
| Leasehold land | 967,009 | 994,855 |
| Right of Use assets | 2,669,129 | 5,998,854 |
| Other financial assets | 428,000 | 634,000 |
| | **140,943,027** | **148,940,619** |
| **Current assets** | | |
| Inventories | 103,507,384 | 86,107,493 |
| Trade receivables | 60,698,079 | 50,847,000 |
| Other short-term operating receivables | 14,974,204 | 19,540,157 |
| Other financial assets | 600,000 | 600,000 |
| Cash and cash equivalent | 72,379,452 | 58,774,862 |
| | **252,159,119** | **215,869.512** |
| | | |
| **TOTAL ASSETS** | **393,102,146** | **364,810,131** |
| | | |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Equity** | | |
| Authorised, issued and fully paid-up share capital | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Retained earnings | 275,973,475 | 245,519,940 |
| **TOTAL EQUITY** | **279,571,937** | **249,118,402** |
| | | |
| **Non-current liabilities** | | |
| Lease liabilities | 2,971,881 | 6,145,443 |
| Employment benefit liabilities | 5,710,604 | 5,545,983 |
| Provision for quarry site restoration | 4,721,748 | 3,778,949 |
| Deferred income tax liability | 8,624,404 | 10,435,603 |
| | **22,028,637** | **25,905,978** |
| **Current liabilities** | | |
| Lease liabilities | | |
| Current income tax payable | - | 769,868 |
| Trade and other payables | 88,607,281 | 86,247,190 |
| Dividend payable | 2,894,291 | 2,768,693 |
| | **91,501,572** | **89,785,751** |
| **TOTAL LIABILITIES** | **113,530,209** | **115,691,729** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **393,102,146** | **364,810,131** |

217500402

Nipashe
TESA
Jumanne Julai 18, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Mafunzo kukabiliana na majanga ya moto hayabagui ni kwa wote



Ukurasa 14

## Mitandao inapokuwa mwalimu wa kufunza watoto maasi, udhalilishaji

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

KUMEKUCHA KIMATIBABU

# Viungo vya maiti vyapandikizwa wagonjwa, wapona maisha yaendelea

WAKATI Afrika hata Tanzania mtu anaweza kufa kwa kukabwa na chakula kooni, Ulaya viungo vya marehemu vinatumiwa kuponya wagonjwa na maisha kuwa safi na kazi zinaendelea.

Ni uvumbuzi wa kuviamsha na kuvipandikiza viungo vya marehemu kwa wagonjwa ili kuokoa maisha yao, mbinu mpya inayopinga ikidaiwa haina maadili.

Wanaopinga inasemekana msimamo wao ni kuwa kuchukua viungo vya maiti ni kinyume na sheria, kwa mfano, moyo wa mtu aliyekufa unapotolewa na kupachikwa kwa binadamu mwingine, ni kama marehemu anaanzishiwa tena mzunguko wa damu, licha ya kwamba mwili unaopokea damu siyo wake.

Mashine hutumiwa ili kuangalia kama moyo au kiungo kingine hunafaa kwa ajili ya kupandikizwa kama kiungo na unapofanyakazi mgonjwa hupatiwa na kuwa tiba sahihi kwa tatizo lake.

Wapo wanaopinga wakidai ni kuwafufua wafu, wanapinga kuwa kufanya hivyo hakuvutii, huku wengine wakihoji maadili yanatumikaje hapo?

Mgonjwa Anthony Donatelli (41), alikuwa amelazwa hospitalini akisubiri viungo, kijana huyo anayeishi San Diego, California Marekani, anasema ana ugonjwa wa 'amyloidosis' unaosababisha mkusanyiko wa aina fulani za protini zisizo za kawaida katika mwili.



Upasuaji wa moyo ukiendelea hospitalini. PICHA: MTANDAO

Tiba yake ilikuwa kupata viungo vitatu na siku ilipotimia Februari mwaka jana, akawa mtu wa kwanza duniani, kupandikizwa moyo, ini na figo,

Tiba hiyo ya kutumia viungo vya wafu aliyopatiwa hutumia mbinu inayoitwa 'BRN normothermic regional perfusion.'

Leo anafurahia maisha yake na familia yake, amepona, Donatelli, sasa anaishi anaendelea na maisha baada ya kustaafu jeshini.

**KIFO Vs MAISHA**

Bila shaka, si kila mtu anakubaliana na maoni ya kubandika viungo vya marehemu kwa mtu aliye hai.

Madaktari wengine wanapinga mbinu ya BRN, hasa kuhusiana na upandikizaji wa moyo, kwa sababu inahusisha kuingiza damu yenye oksijeni kwenye moyo wa marehemu ili upige tena.

**CHANZO VIUNGO**

Watoa viungo hivyo ni watu walio na magonjwa ambayo hayapo ni mfano ya ubongo usiopona ambao wanaishi kutokana na kupumua kwa msaada wa mashine mawodini.

Madaktari kabla ya kutoa viungo vya watu kama hao, lazima wapate ruhusa na idhini kutoka kwa familia zao.

Kisha mashine za oksjeni zinaondolewa moyo na mapafu vikiacha kufanya kazi, baada ya dakika tano mtu hutangazwa kuwa amekufa.

Baada ya hapo daktari hutumia mashine kuingiza damu ndani ya mwili wa mtu aliyefariki ili kujaribu iwapo moyo na mapafu yake hufanya kazi tena.

Utaratibu huo hutumika kuangalia kama moyo wa mgonjwa unafaa kwa kupandikizwa au la.

Mchakato huu hufanyika kwa haraka iwezekanavyo.

Ingawa BRN imekuwa ikitumika kwa miaka nchini Australia, Uingereza, Ufaransa, Uhispania, Ureno, Italia na Uswisi, mbinu hiyo imezua gumzo nchini Marekani kwa 'sababu za kimaadili'.

Wanaopinga mbinu hiyo, wanasema kuanzisha upya moyo wa marehemu ni sawa na kumfufua mfu. Wasiwasi wao unazidi ukifikia kiasi kwamba Chuo cha Madaktari cha Marekani kilitoa taarifa Aprili 2021 kikihimiza kusitishwa kwa matumizi ya BRN kwa kuzingatia 'maswali mazito ya kimaadili yanayozunguka uamuzi wa kifo'. Taarifa hiyo pia inasema kuwa "mbinu ya BRN zinamfufua mgonjwa aliyekufa ni jambo linaloibua tafakari.

Binadamu anayeacha kupumua anatangazwa kuwa amekufa na ni sheria ya asili au maumbile kwamba kifo hakiwezi kubadilishwa.

Hoja kuu ya wapinzani wa BRN ni kwamba kuhuisha (kuamsha) moyo wa marehemu au maiti ni ukiukwaji mkubwa wa sheria za maumbile.

Mashirika kadhaa ya kupokea viungo vilivyotolewa kama mchango au usaidizi (OPOs) yanakubaliana na hoja hii.

Alexandra Glazier, akizungumzia BRN anasema "lengo letu kuu ni kuhakikisha kuwa haki za waliochangia viungo au wale walioaga dunia zinaheshimiwa."

Shirika la Alexandra 'New England Donor Services' kwa sasa linafanya tiba ya mfumo wa BRN kwa ajili ya upandikizaji wa viungo vya tumbo.

**UNAWEZA FUFUA?**

Hakuna anayeweza kufufua

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mafunzo kukabiliana na majanga ya moto hayabagui ni kwa wote

## Jeshi Zimamoto na Uokoaji lafikisha elimu kwa wanaoishi na ulemavu

NOVEMBA 22 mwaka jana, ni tarehe inayoacha historia ya simanzi kwa baadhi ya familia za watoto kadhaa wenye mahitaji maalumu, waliokuwa wanafunzi katika Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi, ni baada ya kupoteza maisha.

Ilikuwa saa 4:00 usiku wanafunzi watatu walifariki dunia baada ya bweni lao kuteketea. Walikuwa wamelala watoto 32 ambao baada ya kutokea janga hilo 29 walinusurika kwa kukimbilia nje lakini watatu ambao ni vipofu walishindwa lakini walikosa msaada na kufariki dunia.

Buhangija Jumuishi iliyopo Manispaa ya Shinyanga, inatoa elimu kwa watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu, wenye mahitaji maalumu kutoka maeneo mbalimbali kama mikoa ya Simiyu na Tabora, wote huishi bwenini.

Idadi ya wenye ulemavu wanaosoma shuleni hapo na kuishi bweni ni 197, viziwi wakiwa 84, wasioona 30, ulemavu wa viungo wanne, uoni hafifu mmoja na wenye ualbino 78, anasema Mwalimu Mkuu Fatuma Jilala.

Anakumbusha majina ya waliopoteza maisha katika ajali hiyo ya moto kuwa ni Niliam Limbu (12), Careen Mayenga (10) na Catherine Paulo (10) wote wa darasa la kwanza.

Anasema walishindwa kujiokoa na kuokolewa kwa sababu za upofu lakini walimu pamoja na walezi hawakuwa na elimu ya namna ya kukabiliana na majanga ya moto na vifaa vya uokozi lilikuwa tatizo pia.

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Shinyanga, Inspekta Stanley Luhwago, anasema kila mmoja anahitaji kufahamu jinsi ya kujiokoa na kujinusuru na ajali kama za moto.

Anasema ni kwa mustakabali huo, wametoa elimu ya kukabiliana na majanga ya moto katika shule hiyo ya Msingi Buhangija Jumuishi, ili likitokea tena tatizo bweni kuwaka moto wanafunzi, walimu na wasaidizi wengine waanze kuuzima katika hatua za awali na kuokoa maisha ya watoto.



Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wilaya ya Shinyanga, Stanley Luhwago, akitoa elimu kwa vitendo namna ya kukabiliana na majanga ya moto kwa walimu na walezi Buhangija Jumuishi. PICHA: MARCO MADUHU

Anasema shule nyingi za bweni zinahitaji kupewa elimu ya kukabiliana na majanga hayo, ndiyo maana wameamua kuelimisha pia katika shule hiyo ambayo ina wanafunzi wenye ulemavu na wanaoishi bweni ili siku moto ukitokea tena usilete madhara na vifo.

"Tumewapa elimu walimu na walezi ya kukabiliana na kuwafunza namna ya kutumia vifaa vya kuzimia moto (fire extinguishers), blangeti zito kufanya uokozi kwa watoto kabla moto haujawa mkubwa,"anasema Luhwango.

Anataja vyanzo vya moto nyumbani na sehemu kama shule kuwa vinaweza kuwa vinatokana na hitilafu ya umeme, uchakavu wa miundombinu ya umeme ndani ya majengo, matumizi mabaya ya umeme, kutumia vifaa feki vya umeme na hata mafundi vishoka kuwweka miundombinu ya umeme ndani ya jengo.

"Zimamoto tunatoa wito kwa wananchi wajenge tabia ya kuwa na vifaa vya kuzimia moto majumbani, sehemu za kazi, maeneo ya shule na kwenye mabweni, ili moto ukitokea waanze kuuzima kwa hatua za awali, pamoja na kupiga simu bure kwa namba ya dharura 114, ili tufike mapema na kuuzima kupunguza madhara,"anasema Luhwango.

"Tunashukuru kwa mafunzo haya yatakuwa msaada mkubwa kwetu, endapo likitokea tena tatizo la moto tutakuwa na ujuzi wa kuwaokoa watoto hawa wasiteketee na moto kama ilivyotokea," anasema Mwalimu Fatma Jilala.

Ofisa Elimu Kata ya Buhangija, Mackrine Shija, anasema ni faraja kuona Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutoa elimu kwa walimu na walezi wa shule hiyo jumuishi, namna ya kukabiliana na majanga ya moto ili kuwaokoa watoto wenye ulemavu wakati wa majanga.

Edward Mdagata ni Ofisa Elimu Maalumu Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, anawasihi walimu na walezi wa shule hiyo jumuishi, kukabili majanga ya moto kwa kutumia elimu waliyopewa ili siku likitokea tena tatizo la moto waanze kuuzima.

"Shule hii jumuishi ni muhimu kupewa elimu ya kukabiliana na majanga ya moto, sababu ina watoto wenye mahitaji walishapoteza wenzao watatu kwa kuteketea na moto wakiwa wamelala bwenini na kunusurika 29," anasema Mdagata.

Endapo wangekuwa na elimu ya kukabiliana na majanga hayo huenda watoto hao wasifariki dunia, anaongeza.

Mwalimu Elizabeth Matheo, anasema baada ya kupata elimu hiyo wana uwezo wa kuuzima moto katika hatua za awali kwa kutumia 'fire extinguisher' wakati wakisubiri zimamoto kufanikisha kazi ya kuzima kwa ufanisi na kuokoa majeruhi.

Mwalimu mwingine Agnes Makambajeki, anasema hofu inapungua licha ya kupoteza maisha wanafunzi wao endapo likitokea tena tatizo la moto, sababu kwa sasa kila bweni kuna kifaa cha kuzimia moto.

"Kwa sasa angalau tuna elimu ya kukabiliana na majanga ya moto tofauti na hapo awali tulikuwa hatuna kabisa elimu yoyote hata kushika hatujui japo kuwa zimewekwa kila bweni," anasema Makambajeki.

Mwanafunzi mwenye ulemavu Paulo Bundala, anasema walimu na walezi kupewa elimu hiyo ya kukabiliana na majanga ya moto, itasaidia kuokoa maisha yao na vitu vyao endapo likitokea tena tatizo la kuwaka moto kwenye mabweni yao.

"Sisi ni watoto wenye ulemavu ambao tunahitaji uangalizi wa karibu, na wengine hawawezi hata kukimbia endapo likitokea tatizo la moto, kama tulivyopoteza wenzetu watatu wasioona ambao walishindwa kukimbia," anasema Bundala.

# Viungo vya maiti vyapandikizwa wagonjwa, wapona maisha yaendelea

INATOKA UK. 11

mtu aliyekufa, makala iliyoandikwa na wataalamu wa matibabu wa Chuo Kikuu cha New York, Brendan Parent, Nader Mozmi, Arthur Kaplan na Robert Montgomery, ikachapishwa mwaka 2022 katika Jarida la Marekani la Kupandikiza Viungo kama jibu la upinzani dhidi ya mbinu ya BRN na Chuo cha Marekani cha Madaktari.

Makala hiyo inasema ni ukweli kuwa moyo wa mtu aliyefariki huanza kupiga tena moja kwa moja, na kusukuma damu kwenye viungo na hili halibadili ukweli huu.

Pia inasema kuwa matumizi ya mbinu ya BRN hayabadilishi hali ambazo familia na timu ya matibabu hufikia hitimisho kwamba mgonjwa hana matumaini ya kuishi.

"Mbinu ya BRN haimfufui mgonjwa," katika mbinu hii, kurejesha mzunguko wa damu huanza tena ndani ya mwili wa mtoaji kiungo yule aliyekufa lakini ndani ya mtu mwingine, hivyo hafufuliwi. Ni jaribio la "uaminifu, uwazi na heshima" kuokoa kiungo, kwani kifo kiko chini ya sheria za asili au maumbile."

Daktari Nader Mozmi, anasema mtu akifariki kwa ugonjwa wa moyo au mapafu, njia bora ya kujua iwapo moyo wake unafaa kupandikizwa ni kurejesha mzunguko wa damu wakati kiungo hicho kikiwa mwilini.

Mozami, anafanya kazi na mkurugenzi wa upasuaji wa upandikizaji wa moyo na usaidizi wa mitambo ya mzunguko wa damu huko NYU Langone Health, pia anasema tangu aanze kutumia mbinu hiyo mwaka 2020, mioyo iliyoonekana kuwa haifai kupandikizwa haijatumika.

'Cardiac reprogramming' pia ni njia nyingine ya kurejesha uhai wa moyo. Aidha, haina uhusiano wowote na kumfufua marehemu. Haihusishi kufufua mtoaji wa kiungo, kwa sababu kwa maneno ya asili, kuongeza muda au uboreshaji wa ubora wa maisha huitwa kuzaliwa upya.

Anaongeza kuwa familia ya mgonjwa inapoamua kuondoa mashine za kumsaidia mgonjwa kuishi, kifo chake huamuliwa. Kwa hiyo wafu hawafufuliwi. Hii imeeleweka vibaya, lakini ukweli ni kwamba BRN haina maadili kutokana na kuhusisha viungo vya marehemu.

Wakati suala hilo linajadiliwa huko Marekani, mbinu hii inaendelezwa katika nchi kadhaa, majaribio katika suala hili yanafanyika Uswizi, Uholanzi, Norway na Canada.

BBCSWAHILI

ELIMU

NA CLAUDIA KAYOMBO, SINGIDA

# Ufumbuzi wa tatizo la maji shule za Singida unapoanzia Ukombozi



Mwanafunzi akifurahia maji shuleni. PICHA: MTANDAO

LICHA ya kukosekana takwimu za moja kwa moja zinazoonyesha ukubwa wa tatizo la maji kwenye shule za msingi, uhaba wa maji ya kunywa, kunawa na kutumika maliwatoni ni moja ya changamoto kubwa inayotesa wanafunzi shuleni.

Hivi karibuni, Shule ya Msingi Ukombozi iliyopo Manispaa ya Singida inaachana na maisha ya 'kijangwa' ni baada ya kuchimbiwa kisima chenye urefu wa mita 126, anasema Mwalimu Mkuu, Yesaya Ramadhani.

Anaongeza kuwa kimemaliza tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji safi na salama ya kunywa na kusafishia mazingira hasa vyooni.

Mwalimu huyo, anayeeleza kuwa anatarajia kustaafu kazi hiyo mwaka huu, anafurahia kuiachia shule maji ya kutosha, akieleza kuwa mradi ulikamilika Oktoba 2022 na tangu hapo wanafunzi hawana shida tena kwani kuna maji ya kutosha ya kunywa, vyooni, kupikia, ujenzi, kumwagilia mimea na usafi.

"Kabla hali ya maji hapa shuleni haikuwa nzuri, tulikuwa tunatumia maji ya Wakala wa Majisafi na Majitaka Singida (SUWASA) ambayo hayakuwa yanatosheleza, hivyo tukaanzisha utaratibu wa tuwaagiza wanafunzi wafike na maji katika vibuyu. Sasa mkombozi amepatikana," anasema Mwalimu Ramadhan.

Mwalimu huyo mkuu anasema Ukombozi moja ya shule zinazofanya vizuri katika mitihani mbalimbali ukiwamo ya taifa, ina wanafunzi 1,800 na walimu 25, kati ya hao, wawili wapo masomoni.

"Wanafunzi hao 1,800 kwa kutwa wanakunywa mapipa sita kando ya mengine yanayotumika katika usafi, vyooni, kumwagilia miti na maua pamoja na jikoni kupika chakula cha walimu na wanafunzi."

Anaishukuru serikali, akisema maji ni uhai, hivyo kunapokosekana maji watu hawawezi kukaa sehemu moja wakatulia, lakini sasa wanafunzi hawahangaiki tena kutafuta maji, muda wa masomo kama wana kiu wanakwenda kunywa na kurudi tena darasani kwa utulivu.

Anasema pamoja na Ukombozi, serikali ifanye utafiti kubaini shule hususan zile zenye uhaba wa maji zipelekewe ya kunywa kwani ni muhimu na hata katika maandiko matakatifu inaelezwa hata katika vitabu vitakatifu kikiwamo cha Kutoka sura ya 17:3 inayosema: Lakini wote walikuwa na kiu, wakamnungunikia Mose au Musa wakisema, kwanini ulitutoa kule Misri utuue kwa kiu sisi na watoto wetu na mifugo yetu?"

Maneno hayo yanaonyesha umuhimu mkubwa wa maji kwani anayeyakosa kwa muda mrefu anaweza kupoteza uhai.

Wanafunzi wanaonyesha furaha yao wanapolinganisha maisha waliyoishi kabla ya kuanza kutumia maji hayo Oktoba mwaka 2022, na kusema maji na chakula ni masuala muhimu kufikie elimu endelevu.

Rosemary Daniel mwanafunzi wa shule hiyo anasema kabla ya kuletewa maji hayo walikuwa wanalazimika kuja na maji katika madumu ya lita tatu au tano kila siku wanapotoka nyumbani.

Anasema maji hayo walikuwa wanayatumia kumwagilia miti, maua, kunywa na kusafishia madarasa na vyoo vya shule yao.

Rosemary anafafanua kuwa walikuwa wanaweka madumu na ufagio chini msimu wa mvua kwa sababu bustani wakati huo hazikuhitaji maji lakini walilazimika kubeba ya kwao ya kunywa.

Anasema sasa wapo huru hawabebi tena maji kwa kuwa wanayo ya kutosha shuleni kwao, ambayo wanatumia kunywa, kupikia chakula chao, kujengea majengo ya shule, kusafishia madarasa na vyoo pamoja na kumwagilia maua na miti wanavyostawisha shuleni hapo.

"Naishukuru serikali imetuondolea kibarua cha kubeba madumu ya maji shuleni kila siku, naomba itujengee madarasa ya kutosha na ituletee walimu wengi zaidi," anasema Rosemary.

Tajany Makota, anayesoma darasa la saba katika shule hiyo anasema hawahangaiki tena kutafuta maji ya kunywa shuleni hapo wakijihisi kuwa wametua mzigo mzito.

"Naishukuru sana serikali imetuletea maji hapa shuleni, naomba ipeleke pia kwenye shule nyingine ambazo wanafunzi wanahangaika kutafuta maji ya kunywa," anasema Tajany.

Anaotaja Shule ya Msingi Kambarage, iliyoko Halmashauri ya Kibaha mkoa wa Pwani ambayo alikuwa akisoma mwaka jana wakati akiwa darasa la sita anaitaja kwamba ina uhaba wa maji.

> "Kabla hali ya maji hapa shuleni haijawa nzuri, tulikuwa tunatumia maji ya Wakala wa Majisafi na Majitaka Singida (SUWASA) ambayo hayakutosheleza, hivyo tukaanzisha utaratibu wa kuwaagiza wanafunzi wafike na maji katika vibuyu. Sasa mkombozi amepatikana," anasema Mwalimu Ramadhan.

"Wakati nasoma darasa la sita kwenye Shule ya Msingi Kambarage, kulikuwa na shida kubwa sana ya maji, naiomba serikali iwapelekee nao maji kama ilivyotuletea sisi hapa Ukombozi," anasema Makota.

Mwanafunzi huyo anayeshika nafasi ya kwanza katika darasa lake lenye wanafunzi zaidi ya 160 anasema anataka kuwa daktari ili awatibu wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi mbalimbali yakiwamo ya mlipuko yanayosababashwa na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

Analaumu wenzi wa mabomba ya maji, akisema anachofahamu kuwa chanzo cha shule yao ya Ukombozi kukosa maji ni wezi kuiba mabomba ya maji ya kunywa na ya chooni kabla uongozi wa shule hiyo haujaajiri walinzi.

Khairath Muro anaishukuru serikali kwa kuwatua mzigo wa kubeba madumu ya maji shuleni kila siku.

"Sasa hatubebi tena madumu shuleni, serikali imetuondolea mzigo wa kubeba madumu kutoka nyumbani kila siku, naishukuru sana tunaomba Baraka za Mungu kwa walimu wetu ambao wanatufundisha kila siku, viongozi wa serikali na wote waliosaidia kuondoa mzigo wa kubeba maji kutoka nyumbani kuja nayo shuleni kila siku.

"Naiomba serikali ifanye mpango izipelekee maji shule zote ambazo wanafunzi wake wanateseka kutafuta maji ya kunywa na ya kumwagilia maua," anasema Khairath. Akizungumza wakati wa hafla ya kuelezea mafanikio ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, anasema upatikanaji wa maji kwa halmashauri ya manispaa ya Singida umeongezeka kutoka asilimia 58 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 80 mwaka huu.

Kwa upande wa mtandao wa majitaka Serukamba, anasema kwa sasa wakala umeanza kujenga mabwawa ya kutibu majitaka na baadaye upo mpango wa kujenga mitandao ya mabomba ya kukusanyia majitaka kutoka majumbani kwenda kwenye mabwawa.

"Mamlaka ya SUWASA imepatiwa jukumu la kutoa huduma nje ya eneo la manispaa na sasa itaanza kuhudumia maeneo ya miji ya Ikungu, Puma, Sepuka, Irisya, Makiungu, Njiapanda na Ilongelo," anaeleza Serukamba.

Anasifu juhudi za upatikanaji maji vijijini akieleza kuwa umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2020/2021 hadi asilimia 64 sawa na wakazi 955,131 waishio vijijini kufikia Februari mwaka huu.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN,ZANZIBAR

# Mitandao inapokuwa mwalimu wa kufunza watoto maasi, udhalilishaji

- Wanapofikishwa mahakamani wadai ndiyo inayowafunza, hukamilisha kwa majaribio



Mtoto akiwa rafiki wa simu au kompyuta mzazi au mlezi amfuatilie ili kumlinda. PICHA: MTANDAO

KUONGEZEKA udhalilishaji wa kijinsia wa wanawake na watoto ni janga linalochochewa na mengi, lakini teknolojia ya mawasiliano inayokuja na matumizi ya mitandao ya simu, YouTube, televisheni na kukosekana kwa ushirikiano wa wazazi kwenye malezi, vinakoleza tatizo.

Kwa mujibu wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), matukio 1,360 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwaka 2022 na waathirika 1,361 kati ya hao, wanawake ni 185 , watoto ni 1,173, miongoni mwao wasichana walikuwa 889 na wavulana 284.

Aidha, utafiti uliofanywa mwaka 2022 na mradi wa " The Disrupting Harm Project" na Taasisi ya End Violence Against Children, zinaonyesha asilimia 67 ya watoto wa Tanzania wenye umri wa miaka 12-17 ni watumiaji wakuu wa mitandao.

Kadhalika unabainisha kuwa kati ya asilimia 67 ya watoto hao wapenda mitandao, asilimia 26 ni wasichana wenye umri wa miaka 12-13, ambao licha ya kupata vizuizi kutoka kwa wazazi na walezi wao wanaendelea.

Mwenyekiti wa Mahakama za Watoto Zanzibar, Zuwena Abdulkadir, anasema lazima kuwapo kwa matumizi sahihi ya kidijitali katika kutumia mitandao zikiwamo simu ili kunusuru kizazi.

Anasema baadhi ya watoto wanaofikishwa mahakamani wanapoulizwa sababu za kufanya vitendo hivyo vya udhalilishaji, wanajibu kwamba wameona katika mitandao hivyo, lazima kuwapo na udhibiti wa matumizi ya teknolojia ili kuwalinda watoto.

Mwenyekiti huyo anasema wakati umefika watoto watumie mitandao kwa kupata idhini ya wazazi au walezi katika maeneo maalumu na si kila kitu, anafafanua.

"Vitendo vingi vya udhalilishaji wa kijinsia watoto kwa watoto wanavyofanyiwa na baadhi yao ni baada ya kuviona kupitia mitandao ya kijamii hasa kwenye simu au kompyuta" anasema Mwenyekiti.

Fatma Juma, mkazi wa Fuoni mjini Zanzibar, anasema matumizi mabaya ya teknolojia hasa simu yanaendeleza ugumu wa kudhibiti watoto wasijiingize katika vitendo hivyo viovu.

"Jamii haina uelewa wa madhara yatokanayo na mitandao hiyo na baadhi yao huwaachia watoto wao simu na kuangalia mambo yasiokubalika ambayo yamejaa upotoshaji na mmomonyoko wa maadili," anaongeza.

Aidha, baadhi ya watoto hufanyiana vitendo vya udhalilishaji baada ya kuona matukio mbalimbali kupitia simu kutokana na kukua kwa teknolojia hiyo na kuishi familia zisizofuatilia maudhui waliyatazama, anaongeza Fatma.

Sabrina Haji Kombo, Mwenyekiti Baraza la Watoto Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, anaiomba serikali na wadau kuandaa mipango thabiti ya kuwasaidia watoto kupata malezi bora na ulinzi ili waepukane na udhalilishaji na kuangamizwa na mtendo yasiyofaa.

Sabrina anasema watoto wanapaswa kutafuta taarifa zinazowahusu na si mambo mabaya ambayo yatavunja utu wao na kukosa haki zao zinazostahiki kutokana na kupotoka mapema au kuingia katika migogoro ya kisheria na jamii wanazoishi.

"Tutoe taarifa za watu waovu, kutambua haki na wajibu wetu, kupatiwa elimu ya kujitambua na stadi za maisha, itasaidia kutupa mbinu za kukabiliana na changamoto za kijamii, ukatili wa kijinsia na udhalilishaji," anasema Sabrina.

**WANAWAKE WAATHIRIKA**

Mkuu wa Kitengo cha Upelelezi Makosa wa Kimtandao Jeshi la Polisi Zanzibar, Issa Mohamed Salum, anasema hali ya udhalilishaji makosa ya kimtandao ni mbaya na waathirika wakuu ni wanawake.

Anasema ukatili na udhalilishaji wa kupitia teknolojia ya kimtandao ni tatizo kwa sababu watumiaji wingi hawajui sheria na kanuni na taratibu za matumizi salama ya mitandao hivyo hubakia wahanga zaidi kuliko kunufaika.

"Wakati umefika jamii itumie vizuri na kwa usalama mitandao ili kuepuka kubanwa bila kujijua huu ni wakati wa kuwekeza kwenye matumizi ya simu kwa maendeleo ya kiuchumi," anasema.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Mkoa wa Kaskazini Unguja, Salum Khamis Machano, anasema matumizi ya teknolojia kwa watoto na wanafunzi kwa sasa hayaepukiki lakini elimu zaidi inahitajika ili yawe kwa wakati sahihi.

**ELIMU**

Ofisa Elimu Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Juma Mwadini Abdala, anawataka wadau wanaosimamia haki za watoto kwa kushirikiana na serikali kutoa elimu kwa jamii kuhusu sheria inayohusiana na makosa ya kimtandao ili kudhibiti vitendo vya udhalilisha.

Anasema kuna makosa mingi ya udhalilishaji kwa njia ya mtandao lakini hayaripotiwi katika vyombo vya sheria kutokana na jamii kutokuwa na uelewa wa sheria hiyo.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Zanzibar (SUZA), Dk. Sikujuwa Omar, anasema marekebisho na mapitio ya sheria mbalimbali zinazomlinda na kumuhusisha mtoto yanahitaji kupitiwa upya kumlinda ili awe salama zaidi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake TAMWA, Zanzibar Asha Abdi, anawataka wazazi na walezi kuishi karibu na familia zao ikiwamo kuangalia mwenendo wa maisha yao ya kila siku hatua ambayo itakayosaidia kugundua mapema matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Anasema lazima wazazi na walezi kuzingatia matumizi ya simu kwa watoto wao ili kuondosha janga la udhalilishaji kwa watoto linalochochewa na matumizi ya teknolojia.

Aidha, anaishauri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwa na sheria itakayozuia au kudhibiti picha, video na taarifa zenye kwenda kinyume na maadili, silka na tamaduni za Watanzania ili kukabiliana na mporomoko wa maadili na kudhibiti vitendo hivyo.

Anasema kutokana na mabadiliko ya kidunia na wakati TCRA ihakikishe inazuia matumizi mabaya ya mitandao kutokana na kusababisha watoto kuingia katika maeneo isiyostahili lakini pia kutumbukia kwenye mienendo ya kupotoka.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, anasema kumekuwapo na changamoto za matumizi ya simu kwa watoto ambayo yanapelekea kuibuka kwa vitendo vya udhalilishaji.

Waziri huyo anasema wimbi kubwa la wazazi huwaachia watoto kutumia simu za mkononi bila kuzingatia matokeo yanayoathiri makuzi na maendeleo yao, hivyo ni lazima kila mzazi na mlezi azingatie suala hilo.



# Wahitimu vyuo vikuu watakiwa kuwa mabalozi kutetea nchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Singida kimewataka wahitimu wa vyuo vikuu mkoani hapa kuwa mabalozi wa kujibu hoja za wapinzani wanaoibeza serikali kwamba haijafanya maendeleo yoyote katika nchi hii.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, alisema hayo juzi wakati wa mahafali ya wanafunzi hao ambao ni makada wa CCM yaliyofanyika Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida na kuvishirikisha vyuo na vyuo vikuu vyote.

"Mnarudi nyumbani na huko mtakako kuwapo nendeni mkawe mabalozi mkaisemee serikali na chama chetu kwa kushindana kwa hoja na si kupigana dhidi ya watu ambao wanasema serikali yetu haijafanya chochote jambo litakalomtia moyo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan," alisema.

Mlata alisema nchi ya Tanzania imepiga hatua kubwa ya maendeleo katika kila nyanja kwa kutekeleza miradi mbalimbali na kila mwananchi ni shahidi katika jambo hilo.

Alisema wakati anasoma hakukuwa na barabara za uhakika, huduma za afya zilikuwa duni, lakini leo hii kila kona ni maendeleo matupu na kwamba kuna haja ya kujivunia kazi kubwa iliyofanywa na serikali ambayo inatekeleza ilani ya CCM kufanya miradi hiyo.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao watakapokuwa nyumbani wasiende kukaa bure badala yake wafanye kazi yoyote ya kuwaingizia kipato jambo litakalo watofautisha na vijana wengine.

"Mkiwa nyumbani nendeni mkawe wabunifu kwa kufanya kazi mbalimbali, ufugaji, kilimo, ufundi, ususi, biashara ndogondogo na kazi nyingine mtakazoona mnaweza kuzifanya msiiende kukaa bure na kujiingiza katika vitendo viovu na kwa kufanya hivyo mtakuwa mfano kwa vijana wenzenu na kuwaiga," alisema.

Aliwaomba wahitimu hao watakapofika kwenye wilaya zao waende kujitambulisha kwa wenyeviti wa CCM ili wawatambue jambo litakalowafanya watambuliwe na kushirikishwa katika shughuli mbalimbali za chama hicho.

Mwenyekiti wa Seneti Mkoa wa Singida, Masatu Bure, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa na huruma na moyo wa kujali kwa kuwaongezea posho 'Bumu' kutoka Sh. 8,500 kwa siku hadi Sh. 10,000 na kuwa hivi sasa hawahitaji kuandamana tena kudai posho hiyo.

Kaimu Katibu Mkuu wa Seneti, Yohana Edward, alisema jumuiya hiyo ipo imara na hai na wanaendelea kuwahamasisha vijana kutambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na serikali huku wakihimiza kujisajili kwa mfumo wa kielektroniki kwa manufaa ya vijana vya vyuo vikuu.

Alisema mwaka huu wanatarajia kuongeza vyuo vingine ili vijiunge na jumuiya hiyo na kufanya viwe na idadi ya vyuo 13 ndani ya Mkoa wa Singida.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Eliakim Maswi, akizungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za Idara ya Habari Maelezo jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo na mwelekeo wa utekelezaji wa mwaka wa fedha 2023/2024. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima washauriwa kufanya kilimo chenye tija

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WATAALAMU wa zana za kilimo kutoka Shirika la Uzalishaji Mbegu jijini Dodoma (DASPA), wamewataka wakulima kufanya kilimo chenye tija ili kuondokana na umaskini.

Mtaalamu wa zana za kilimo kutoka DASPA, Peter Kihiyo, aliyasema hayo jana kwenye mkutano wa wakulima wa kijiji cha Mroda, wilayani Chamwino.

Kihiyo alisema ili kuondokana na umaskini wakulima wanatakiwa kutumia mbinu bora za kilimo ikiwamo kupanda kwa kufuata mistari kama wataalam wanavyowaelekeza ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Pia, alisema wakati huu ambao serikali imewekeza fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo ikiwamo wataalamu wa hadi ngazi za kata na vijiji ni vyema wakabadili mitazamo yao na kuondokana na kilimo cha mazoea. Alibainisha wakulima wengi wanachukulia kilimo kwa uzito mdogo, lakini ukweli ni kwamba ni sekta kubwa na yenye uwezo wa kumfanya mkulima apige hatua na kuinuka kiuchumi.

Alisema imefika wakati sasa kutumia kamba kupanda kwa mistari badala ya kutupia mbegu ambazo husababisha kupotea na mazao kuota kiholela shambani.

Mtaalamu huyo alisema kuwa sasa kuna zana za kilimo ambazo zimerahisisha kazi ni vyema wakulima wakazitafuta ili kuongeza ufanisi kwenye shughuli zao za za kila siku.

Kihiyo alisema wamekuwa wakitoa mafunzo ya wawakilishi wa vikundi vya wakulima kutoka maeneo mbalimbali ya namna bora ya kutumia zana hizo. Zana za kilimo ni kwa ajili ya kuwasaidia kutoka matumizi ya jembe la mkono ambalo hutumia muda mwingi shambani na kuongeza kila mkulima kupitia vikundi vyao wanapaswa kutafuta zana hizo.

Mwenyekiti wa DASPA, Janeth Wilson, alisema awali kulikuwa na tatizo la uzalishaji mbegu, lakini sasa wakulima wanapewa mafunzo ya uzalishaji ili kuzalisha kwa ajili ya wakulima wengine.

"Tumekuwa tukitoa mafunzo ya matumizi bora ya zana za kilimo hususani mashine ya kupandia na wakulima wamefundishwa namna ya kutumia mashine hiyo," alisema.

Alisema mashine hiyo ni mkombozi kwa wanawake ambao walikuwa wakishinda shambani kutwa nzima lakini sasa hivi wanaweza kupanda kwa kutumia mashine ambayo wanatumia muda mchache kuliko kutumia mikono.

# KKKT yakemea waumini mavazi yasiyo staha kanisani

**Na Elisante John,** SINGIDA

KANISA la Kiinjili la Kikutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kati mkoani Singida, limekemea tabia mbaya na iliyokithiri kwa baadhi ya waumini wake kuvaa mavazi yasiyo na staha kwenye nyumba za ibada.

Mchungaji kiongozi wa kanisa hilo, Melchizedek Kitiku, alitoa onyo hilo juzi kwenye ibada iliyofanyika makao makuu ya KKKT Usharika wa Amani wilayani humo.

Alisema uvaaji mavazi yasioridhisha kwa vijana na watu wazima, kisha kuingia nayo kwenye nyumba za ibada, ni tabia inayopaswa kudhibitiwa kutokana kwa kuwa inakiuka maadili na nidhamu ya Watanzania.

"Baadhi ya mavazi ya waumini, kwa kweli hayafai kabisa kuja nayo na kuingia nayo kanisani huwezi kuubadili uafrika wako kwa mavazi mabaya na kinyume na maadili yetu tuliyozaliwa nayo," alisisitiza.

Alisema kuna mavazi mengine hutumika usiku kwa ajili ya kulalia na mengine kwenye sherehe za usiku, lakini waumini wengine wanakwenda nayo kanisani.

Aidha, Mchungaji Kitiku, aliwataka wakristo kuachana na matumizi ya simu ndani ya nyumba za ibada kwa kuwa inawaondolea usikivu na utulivu kwa washiriki wengine wenye nia ya kumwabudu Mungu.

"Na sasa hivi kutokana na kukua kwa teknolojia, utakuta kwenye simu ya msharika ameisevu Biblia humo, utamwona wakati ibada inaendelea, ghafla yeye anatabasamu na kucheka cheka ovyo kanisani, unamshangaa, kumbe mwenzako anachati na mwenzake, akili yote haipo hapo...hii sio tabia nzuri ndani ya nyumba za kuabudia," alionya Kitiku.



# Kituo cha afya hakina majokofu kuhifadhi miili

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

KITUO cha Afya cha Iyunga kilichopo jijini Mbeya hakina majokofu ya kuhifadhia maiti hali inayowalazimu wananchi wa eneo hilo kwenda kuhifadhi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ama kwenye Hospitali ya Kanda.

Diwani wa Kata ya Iyunga, Mwajuma Tindwa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson ya kusikiliza kero za wananchi katika kata hiyo.

Alisema katika kituo hicho wananchi kwa kushirikiana na halmashauri wamejenga jengo la kuhifadhia maiti na limekamilika kwa kuwekewa miundombinu yote, lakini halina majokofu.

Aliomba serikali iwasaidie kununua majokofu hayo ili wananchi wasihangaike kwenda kuhifadhi miili ya ndugu zao kwenye hospitali za mbali.

"Tunakuomba mheshimiwa Spika utusaidie tupate vifaa hivi, kituo chetu ni kizuri sana na kinatoa huduma zote muhimu za matibabu lakini kukosekana kwa vifaa hivi kunawakwaza wananchi," alisema Mwajuma.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, Clemence Mwandemba, alisema ujenzi wa kituo hicho cha afya umesaidia kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema awali wananchi wa kata hiyo walikuwa wanalazimika kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya na katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa hata kama magonjwa ni ya kawaida.

Alisema baada ya kituo hicho kukamilika sasa hivi wananchi hao wanatibiwa hapo nahata huduma za upasuaji zinapatikana, lakini tatizo lililobaki ni kukosa majokofu kwenye jengo la kuhifadhia maiti. "Kwenye kituo chetu huduma mbalimbali zinapatikana, ukienda pale hata huduma za upasuaji zipo kwa hiyo tunaishukuru serikali kwa jitihada zake za kusogeza huduma kwa wananchi," alisema Mwandemba.

Akizungumza na wananchi hao, Dk. Tulia aliahidi kufuatilia ili vifaa hivyo vipatikane haraka na wananchi wawe wanahifadhi miili ya ndugu zao hapo badala ya kupeleka maeneo ya mbali.

Alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali kuboresha huduma za afya ikiwamo ujenzi huo wa vituo vya afya, zahanati na hospitali za wilaya katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema katika Jiji la Mbeya kulikuwa hakuna hospitali yenye hadhi ya wilaya, lakini katika kipindi ambacho yeye amekuwa madarakani wameshajenga hospitali ya wilaya ambayo tayari imekamilika na inatoa huduma.

Alisema hospitali hiyo ya Igawilo imejengwa na serikali kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 1.5 itazipunguzia mizigo hospitali ya kanda na mkoa.

"Hospitali imekamilika ina kila kitu, ina vifaa vya kutosha, ina watumishi wa kutosha na inatoa huduma zote muhimu, ukitoka hapa kwenye kituo cha afya unakwenda kule na unapata huduma vizuri," alisema Dk. Tulia.

Alisema serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu mingine ikiwamo ya barabara ili wananchi wasafiri kwa urahisi kwenda kupata huduma za afya na huduma zingine kwenye maeneo ya jiji hilo.

Kituo cha Afya Iyunga ni miongoni mwa vya kwanza kujengwa katika jiji hilo, lakini kukosekana kwa vifaa vya kuhifadhia maiti imekuwa kero kwa wananchi.



Waumini wa Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki (KKM) Dayosisi ya Nyanda za Juu Kusini wakiwa kwenye maandamano wakati wa maadhimisho ya mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwa kanisa hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali kuendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amesema serikali inaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji ili kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Mahundi aliyasema hayo jijini hapa kwenye mkutano wa hadhara wa Chama Cha Mapinduzi kuwa serikali imenunua zaidi ya mitambo 25 ya kuchimbia visima vya maji na kuisambaza kwenye kila mkoa.

Alisema kati ya mitambo hiyo, mitano imetengwa kwa ajili ya kuchimbia mabwawa kwenye maeneo ambayo yanakabiliwa na ukame mkali kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha Watanzania wanaondokana na tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji kwa kupatikana karibu na makazi yao.

"Tunaendelea kutekeleza dhana ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani kwa huduma hiyo kupatikana jirani na makazi, mitambo tuliyonunua tayari inafanya kazi kwenye maeneo mbalimbali," alisema Mhandisi Mahundi.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya mtambo uliopelekwa tayari upo katika Wilaya ya Chunya, ukiendelea kuchoronga visima kwenye maeneo yenye uhitaji.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea na harakati za ujenzi wa mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira ambao utakuwa suluhisho la tatizo katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

# TARI yagawia miche ya migomba 3,000 bure wakulima

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imegawa bure miche zaidi ya 3000 ya migomba ya kisasa kwa wakulima wa zao hilo wilayani Rungwe ili kuboresha kilimo cha zao hilo.

Aina nne za miche hiyo iliyofanyiwa utafiti zilianza kugawa na wataalamu wa TARI kwa wakulima na kupatiwa elimu ya njia bora za upandaji wa zao hilo.

Mtafiti wa matunda kutoka TARI Uyole, Daud Mbongo, alizitaja aina ya mbegu ambazo wamewagawia wananchi kuwa ni Tariban moja, Tariban mbili, Tariban tatu na Taribani nne ambazo zimefanyiwa utafiti na kubainika kuwa zinastawi vizuri.

Alisema miche hiyo ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na magonjwa mbalimbali ikiwamo mabaka meusi na minyoo ya mizizi ambavyo ni visumbufu vikuu vinavyoshambulia zao hilo na kupunguza uzalishaji.

Vilevile, alisema mbegu hizo zina uwezo wa kuzaa mikungu mikubwa na hivyo kuwa na faida kubwa kwa wakulima kuliko miche ya asili ambayo wamekuwa wakiitumia miaka yote.

"Ndizi hizi ni za kupika aina ya matoke, zinazaa mikungu yenye uzito kuanzia kilo 30 mpaka 60 kwahiyo wakulima wakizitumia wataongeza uzalishaji nahata kipato chao kitaongezeka maradufu," alisema Mbongo.

Mtafiti huyo alisema sababu ya kuigawa miche hiyo katika Wilaya ya Rungwe ni kutokana na zao hilo kupewa kipaumbele zaidi na wakulima wa eneo hilo kuliko maeneo mengine.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Rungwe, Juma Mzala, alisema aina hiyo ya migomba itakuwa endelevu kwa kuendelea kusambaza machipukizi ili kuendelea kutanua kilimo cha zao hilo.

Alisema aina hiyo ya migomba itasaidia kupunguza magonjwa na visumbufu vingine na aina hiyo ina uwezo mkubwa wa kukinzana na matatizo hayo.

Alisema migomba ya asili ambayo wananchi walikuwa wakiitumia siku zote inakabiliwa na minyoo fundo ambayo inapunguza tija kwenye uzalishaji.

"Sasa hivi migomba yetu asilimia 30 inakabiliwa na minyoo fundo, mbegu mpya zina uwezo wa kukinzana vizuri na tatizo hili, kwa hiyo leo tumeanza kugawa miche hii na tutaendelea mpaka iwafikie wakulima wote," alisema Mzala.

Alisema asilimia kubwa ya wakulima wa Wilaya ya Rungwe wanalima ndizi na hata chakula kikuu kwa wananchi hao ni ndizi.

Mratibu wa Uhawilishaji wa teknolojia wa TARI Uyole, Lusungu Paul, aliwataka wakulima kuzingatia maelekezo ya wataalamu kuhusu uzalishaji wa zao hilo hasa nafasi kwenye upandaji.

Alisema wakulima wakizingatia mbinu za kilimo bora kuna uwezekano wakafikia tija ambayo inatarajiwa kulingana na utafiti uliofanyika wa mbegu hizo.

Mmoja wa wakulima wa Wilaya ya Rungwe waliogawiwa miche hiyo, Elizabeth Sekile, aliwashukuru wataalamu kutoka TARI kwa kuwapatia mbegu hizo za kisasa ambazo alisema zitawasaidia kuongeza uzalishaji.

Aliiomba serikali kusimamia vizuri bei na taratibu za uuzaji wa ndizi kutokana na kuwapo baadhi ya wanunuzi ambao wanahujumu wakulima.



# ACT-Wazalendo yatoa kasoro Sheria ya Ukodishwaji Ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema sheria ya ukodishwaji wa ardhi kwa wawekezaji haina manufaa kwa wananchi na inarudisha nyuma maendeleo tangu serikali ilipofungua uwekezaji kwenye sekta ya utalii visiwani Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, wakati akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho katika kiwanja cha Mkwajuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Makamu huyo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Zanzibar, alisema utaratibu wa serikali kuchukua ardhi na kuwapa wawekezaji badala ya wananchi wenyewe kuingia makubaliano na wawekezaji siyo utaratibu mwafaka katika kumwinua mwananchi kupitia ardhi yake.

Alisema pamoja na Zanzibar kufungua mlango wa uwekezaji bado wananchi waliokuwa wakimiliki ardhi katika maeneo ya fukwe hawajanufaika na uwekezaji kutokana na serikali kuchukua maeneo hayo na kuwapatia wawekezaji badala ya wananchi kunufaika moja kwa moja na rasilimali hiyo.

"Wananchi bado hawajanufaika na rasilimali ya ardhi kutokana na serikali kuchukua maeneo yao na kuwapa wawekezaji wakati wananchi ndio walitakiwa kuingia mikataba na wawekezaji na serikali ibakie kukusanya kodi katika miradi jambo ambalo lingewainua kiuchumi.

Alisema malengo ya chama cha ACT ni kuhakikisha ardhi inamnufaisha mwananchi na serikali haitohusika na ukodishwaji wa ardhi ili kuwapa nafasi wananchi wanaomiliki ardhi waweze kunufaika moja kwa moja kupitia sekta ya uwekezaji na serikali itabakia kukusanya kodi katika miradi itakayoanzishwa.

Akizungumzia kero ndani ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, alisema marais wawili wastaafu walifanya kazi nzuri ya kuitetea maslahi ya Zanzibar ndani ya muungano huo, akiwamo Rais mstaafu Dk. Salmin Amour Juma na Dk. Amani Karume.

Alisema Dk. Salmin aliweza kusimama imara na kuhakikisha Zanzibar inaanzisha kampuni ya simu ya Zantel ambayo ilipata vikwazo katika usajili wake kutokana na suala hilo kuwa chini ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano, lakini alifanikiwa.

Aidha, alisema Rais mstaafu Amani Karume alisimama imara kutetea maslahi ya Zanzibar katika Muungano ikiwamo suala la mafuta na gesi kuondolewa katika orodha ya mambo ya muungano.

Naye Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Ismail Jussa Ladhu alisema, Zanzibar inahitaji rais mwenye uwezo wa kutetea maslahi ya Zanzibar ndani ya Muungano ikiwamo kurejesha kiti cha Zanzibar Umoja wa Mataifa.

Alisema Zanzibar haiwezi kupata maendeleo bila ya kuwa na mamlaka kamili katika mfumo wa Muungano ili kujiamulia mambo yake ikiwamo mipango ya kiuchumi.

Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake Taifa ya Chama hicho, Pavu Juma Abdalla, alisema usimamizi mbovu wa Sheria za Ardhi umekuwa ukiwaathiri wanawake zaidi kwa vile ndiyo wanaoshiriki katika shughuli za kilimo visiwani humo.

Alisema sheria inahitaji kuangaliwa upya ili kuwapa fursa ya kumiliki ardhi wanawake kwa vile ndio wazalishaji wakubwa katika mazao ya kilimo, lakini wana vikwazo vikubwa katika umiliki wa ardhi Zanzibar.

Chama cha ACT-Wazalendo kinaendelea na mikutano yake ya hadhara katika mikoa mitano ya Zanzibar huku suala la kukosoa ufisadi katika miradi ya ujenzi na ubinafsishaji wa Bandari ya Malindi yakiendelea kuwa na mjadala mkubwa katika mikutano hiyo.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, akimjulia hali mzee wa chama hicho, Mauld Machano Adib, alipofika nyumbani kwake Nungwi, wakati akiwa katika ziara ya kuwajulia hali wagonjwa na kuwafariji waliofikwa na msiba. Wa pili kulia ni Mke wa Othman, Mama Zainab Kombo Shaib. **PICHA: OFISI YA MAKAMU**

# Bodi yafafanua mikopo ya wanafunzi wanaosoma nje

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BODI ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar imesema kuwa haitotoa mkopo kwa mwanafunzi yeyote kwenda kusoma elimu ya juu katika vyuo vya nje ya nchi kwa kozi ambayo inapatikana katika vyuo vya Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar, Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Iddi Haji alisema, nafasi za vyuo vya nje itaruhusiwa kwa maeneo ambayo fani zake hazipatikani Tanzania.

"Tanzania tuna vyuo vya elimu ya juu karibu 68 kwa hivyo kozi mbalimbali zinapatikana, kwa wale ambao kozi zao hazipatikani vya kutosha au nafasi zipo chache ndiyo tutaoruhusu kwenda kusoma nje, lakini mkazo zaidi tunakazania kwa vyuo vyetu vya ndani," alisema Mkurugenzi huyo. Alisema hivi sasa Kiswahili kimepanda chati na kinakwenda kuwa lugha ya Afrika na ili kuzalisha walimu wa kutosha kimependishwa chati na bodi hiyo inatoa mkopo pia kwa kozi ya ualimu ikiwamo Kiswahili ili kuzalisha wataalamu wengi wa Kiswahili. "Imebidi Kiswahili tukipandishe chati awali kilikuwa ni daraja la tatu sasa ni lugha ya Afrika Mashariki hivyo ukichukua kozi ya ualimu ikiwamo Kiswahili, Kiingereza na historia kwetu sisi, wewe ni mtaalamu lazima upate mkopo kama anavyopata daktari, mhandisi na mwalimu wa sayansi," alisema.

Alisema wanahitaji kuzalisha wataalamu wa kutosha wa Kiswahili ili kupelekwa katika nchi mbalimbali ikiwamo Zambia, DRC Congo na Afrika Kusini kufundisha Kiswahili kwa sababu Tanzania ndiyo chimbuko la Kiswahili.

Akizungumzia juma la elimu ya juu, Naibu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, alisema itaanza Julai 30 hadi Agosti 5, mwaka huu, ambayo yatafanyika katika viwanja vya Maisara na lengo lake ni kuvikutanisha vyuo vyote vya Tanzania ambavyo huonesha huduma wanazotoa.

Alisema kutakuwa na utaratibu wa kuwasaidia wanafunzi jinsia ya kuomba mikopo katika Bodi ya Elimu ya Juu na kutoa uelewa kwa wanafunzi jinsi ya kujiunga na chuo kikuu na kuchagua kozi zinazoendana na masoko. Aidha, aliwataka wananchi na wanafunzi kutumia fursa hiyo ya kutembelea maonesho hayo ili kujifunza mambo mbalimbali ikiwamo uombaji wa mikopo wa kujiunga na elimu ya juu.

# SMZ kupata mkopo bil. 470/- miradi maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imetangaza kukamilika kwa taratibu zilizowezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kupata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 200 (Sh. bilioni 470).

Fedha zinazotokana na mkopo huo zitasaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii pamoja na miundombinu malengo yakiwa ni kuboresha maisha na hali ya kiuchumi kwa Wazanzibari.

Akizungumza Ikulu Zanzibar, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema huo ni ushirikianao wa aina yake na benki imeweza kufanya kazi na SMZ katika jitihada za kufanikisha miradi ya maendeleo kwa ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Alisema NBC inafurahi kusaidia upatikanaji wa mkopo huo utakaosaidia SMZ kufikia malengo yake ya ukuaji wa uchumi na maendeleo jumuishi.

Sabi alisema mkopo huo ni hatua kubwa na muhimu katika kushirikiana pamoja kwenye malengo ya maendeleo endelevu na kuboresha maisha ya wananchi wa kisiwa cha Zanzibar.

Kadhalika, NBC itaendelea kuwa mstari wa mbele kusaidia jitihada za kuleta maendeleo ya kiuchumi kupitia huduma za kifedha.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi aliishukuru benki hiyo kuweza kufanikisha mkopo huo ambao alisema utakuwa na mchango mkubwa katika kufadhili miradi ya maendeleo Zanzibar.

Alisema mkopo huo utaiwezesha Zanzibar kufikia malengo yake ya kuboresha maisha ya wananchi wake kwenye njanja za kijamii na kiuchumi.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo yatanufaika na fedha hizo kuwa ni huduma za afya, elimu, miundombinu ya usafiri na miradi ya maendeleo ya kijamii.

"Kwa kuwekeza kwenye sekta hizi muhimu SMZ inalenga kuboresha maisha ya wananchi wake na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na kuwezesha kufikia malengo ya muda mrefu ya maendeleo ya kiuchumi," alifafanua.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

THIS CHANGE OF NAME DEED is made this 14th day of March 2022 by me RHODA STEPHEN CHACHA formerly known as RHODA ROBERT THOBIAS a resident of Dar es salaam, now or until recently called RHODA STEPHEN CHACHA.
WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED as follows:

- I absolutely renounce and abandon the use of my said former names of RHODA ROBERT THOBIAS and I assume and determine to take and use the new name of RHODA STEPHEN CHACHA in substitution of my former names of RHODA ROBERT THOBIAS.
- AND IN PURSUANCE of such change of name(s) as aforesaid I DECLARE I shall at all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of RHODA STEPHEN CHACHA in substitution for my former names of RHODA ROBERT THOBIAS so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by the aforesaid former names, but by the new name of RHODA STEPHEN CHACHA only.
- AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE all persons at all times to describe and address me by the new name of RHODA STEPHEN CHACHA.

IN WITNESS whereof I have hereunto subscribed my new name of RHODA STEPHEN CHACHA, and have affixed my signature the day and year herein written.



---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika wilaya ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na 1001/ 2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU THERESIA EMMANUEL MASSAWE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ARDESIA KIMARO MASSAWE**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 8 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 14 Mwezi 7 Mwaka 2023

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA**
**WILAYA YA ILEMELA**
**SHAURI LA MADAI YA PESA NAMBARI 275/2023**
**MDAI............ 1. AYOUB RASHID**
**2. DOTTO MASUKE**
**DHIDI YA**
**MDAIWA .........LEOBINI PASTORY @ MJUNI**

**KWA: LEOBINI PASTORY @ MJUNI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
**POPOTE PALE ULIPO**

Fahamu kwamba wadai wameleta madai yao Mahakamani dhidi yako. Madai haya yamepengwa kusikilizwa tarehe 24/07/2023.
Fahamu kwamba unatakiwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe siku hiyo bila kukosa. Kutohudhuria kwako kutaifanya Mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo na kulitolea uamuzi.
Imetolewa kwa amri na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 17/07/2023

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA
MWANZA.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.02/2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE LENA TOM NDEMELE**
**AND**
**In the matter of application for letters of Administration by CHRISTINA NGENGE MWAJA ..................PETITIONER**

**GENERAL CITATION [RULE75]**
All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are here by cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate [or letter of administration] is made to the above named petitioner.
Objections to the grant shouldbe filed on or before the 20 of july 2023
Date at kyela this 15 june 2023.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MTWARA**
**ILIYOPO MTWARA**
**(EXTENDED JURDICTION)**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 24/2019**
**(Asilia shauri la jinai Na. 1/2014, Mahakama ya Wilaya ya Mtwara)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA...MRUFANI**
**DHIDI YA**
**MUSSA MALYANGO BUSOGO & WENZAKE...MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA: MUSSA MALYANGO BUSOGO – KIMARA KILUNGULE – DSM**
**GERDAT LUKAS MMUNI – KONGOWE – DSM**
**HAMIDU ABDALLAH NGUNDE – MTONI KWA AZIZI – DSM**
**BONIFANCE KOSAINI BUSOGO – KIMARA KOROGWE – DSM.**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE 20/7/2023 SAA 3:00 ASUBUHI BILA KUKOSA.
KUMBUKA KKUKWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 5/7/2023.

F. R. LUKUNA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

---

## TANGAZO GARI LINAUZWA

Gari aina ya **TOYOTA HILUX** lenye namba za usajili **T164DXV** linauzwa lipo katika hali nzuri.

**Taarifa za Gari**

Aina ya gari: **Toyota Hilux**
Mwaka wa kutengenezwa gari: **2004**
Mafuta inayotumia: **Diesel**
Model Namba: **KF-LN167**
Uwezo wa injini: **2980**
Aina ya bodi: **Station Wagon**
Rangi ya gari: **Multi Colour**
Chesesi namba: **LN1670032032**
Namba ya injini: **5L5506667**
Kilometa ilizotembea: **110197**




**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**Piga: 0757823350 / 0692793423**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 62 LA 203**
**PATRICK NGILOI ULOMI MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**HALIMA MOHAMED MAMUYA MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**HALIMA MOHAMED**
**MAMUYA**

**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

PATRICK NGILOI ULOMI Amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lilipo Kinondoni ( Mwananyamala) .Shauri husika limepangwa kutajwa tarahe 20/7/2023 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh SILAS.J. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 14.Mwezi 07 mwaka2023

.,...... ...
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CONJESTA JOSEPH MALLYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 702 AUH** aina ya **SUBARU** yenye CHASSIS NO: **TT2211557** na ENGINE NO: **EN07.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/THE/RB/236413/2023.**

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**GABRIEL MAHEMED KALINGA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE150314** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam, Muda wa kuisha matumizi yake tarehe 26/07/2029. Yeyotea atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MDL/RB/2198/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 36 YA MWAKA 2023**
**INNOCENT BENEDICT**
**MBERESERO..............................................................MDAI**
**DHIDI YA**

1. **FRANK THOMAS NYILIKA ............................................MDAIWA**
2. **VGK CO. LTD ..............................................................MDAIWA**
3. **THE JUBILEE INSURANCE COMPANY OF TANZANIA..........MDAIWA**

**FRANK THOMAS NYILIKA,**
**Phone No. 0658 606355**
**DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI.**

Kwa kuwa Mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za Madai zinazopatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 19/07/2023 saa tatu kamili (9:00) asubuhi mbele ya MHE. JAJI POMO, kwaajili ya kutajwa.
**ANGALIA :**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 21/06/2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
DAR ES SALAAM

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 4 /2023**

**ALEX MGENDA...............................MLETA RUFAA**
**DHIDI YA**
**SALIM EDSON.........................MJIBU RUFAA**

KWA : **SALIM EDSON**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuliwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe **7/8/2023** siku ya Jumatatu saa **3.00** asubuhi ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
**ELEWA KWAMBA,** ukikosa kufika Mahakamani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **10/7/2023**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA.

---

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MCHANGANYIKO

# CHADEMA yajiweka kando mabadiliko Sheria Uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema hakiko tayari kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi, kikisisitiza msingi wa tatizo uko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Kimesema kunahitajika mabadiliko ya mfumo na uongozi kupitia katiba na kupatikana mpya, ili kulifanya taifa kuondokana na ugumu wa maisha, bunge lililodai ni butu na tume isiyo huru.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, alisema jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Zingiziwa, Chanika jijini Dar es Salaam, kuwa kuna haja mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya kufanywa haraka ili nchi iwe na tume huru ya uchaguzi na si vinginevyo.

"Katiba mpya itaondoa sintofahamu ya masuala mengi pamoja na mikataba ya nchi inayotiliwa shaka. Rais ana kinga kubwa, tunahitaji katiba mpya yenye kumpunguzia Rais mamlaka, kama sasa tunaona mikataba inatiwa saini ya bandari, lakini inaacha maswali mengi. Tatizo ni katiba tuliyonayo.

"CHADEMA tumeandikiwa barua hadi tarehe 20 Julai mwaka huu, tuwe tumetoa maoni kuhusu marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi, ili kuwapo uchaguzi huru na haki. Lakini chanzo kikuu ni katiba. Katiba ya mwaka 1977 inasema Rais ana mamlaka ya kumteua Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, tafsiri yake ni kwamba tatizo lipo katika Katiba.

"Huwezi kutatua matatizo haya bila katiba mpya. Hawa watu wanatupa matumaini hewa. Mimi kama mtendaji mkuu wa chama, ninasema hatuhangaiki kupeleka mapendekezo ya kufanyia marekebisho ya sheria ya uchaguzi, kwamba ndiyo tutapata uchaguzi huru na wa haki, hatuko tayari," alisema Mnyika.

Alisema viongozi wa CHADEMA wataendelea kuzunguka nchi nchi nzima kuelezea mkataba wa bandari hadi utakaporudishwa bungeni na kujadiliwa upya, ili uwe na maslahi ya kitaifa.

"Mbunge wa jimbo hili anaacha kuja kuongelea kuhusu bandari katika jimbo lake, anakwenda katika vyombo vya habari. Ninasema huyu mwondoeni wakati ukifika, wananchi mna uwezo huo," alisema Mnyika.

Aliongeza: "Wananchi wanapitia changamoto kadhaa, ikiwamo gharama za maisha kupaa na bidhaa ni ghali. Tunahitaji kukutana ili tujadili, kwa mustakabali wa nchi yetu."

# Mvutano wa kisiasa wazidi kushuhudiwa Kenya

**NAIROBI,** KENYA

MVUTANO wa kisiasa umezidi kushuhudia Kenya baada ya upinzani kutangaza kufanya maandamano mengine kwa siku tatu mfululizo kuanzia kesho, huku wanasiasa wanaokinzana wakiendelea kuvutana hali inayotishia kutokea vurugu wakati wa maandamano hayo. Akizungumza katika moja ya mikutano aliyoifanya mwishoni mwa juma lililopita, Waziri wa Mambo ya Ndani, Kithure Kindiki, aliapa kuwa idara za usalama zitawashughulikia kikamilifu aliowaita wahalifu wanaojificha nyuma ya kivuli cha katiba.

Juma lililopita Rais William Ruto, alimuonya kinara wa upinzani Raila Odinga, akisema maandamano ya wiki hii hayatakubalika na wahusika watakabiliwa na mkono wa sheria, ikiwa ni baada ya yale ya wiki iliyopita kushuhudia vurugu zilizosababisha watu 13 kupoteza maisha.

"Ndugu zangu wa upinzani tafadhali tufanye siasa kwa amani tuuze sera zetu, sijasema mkubaliane na serikali na wale wanaounga mkono msilazimishe watu wakubaliane na sera zatu, wako na uhuru wa kuwa na maoni tofauti," alisema Kindiki.

Vyama vya walimu nchini Kenya, pia vilitoa wito kwa Rais Ruto na kinara wa upinzani, Raila Odinga kufanya mazungumzo na kusitisha maandamano ambayo yamepangwa kufanyika siku tatu kila wiki, vikieleza kuwa maandamano hayo yamesababisha kuathirika kwa masomo.

Kando na vyama vya walimu, viongozi wa kidini pia walitoa wito kwa pande hizo mbili kufanya mazungumzo na kumaliza mzozo uliopo kwa sasa unaotishia kulitumbukiza taifa hilo la Afrika Mashariki katika mzozo.

Aidha, ilielezwa kwamba upinzani ulisisitiza kuwa maandamano yake yataendelea kama ilivyopangwa licha ya onyo kutoka kwa serikali kuwa haitaruhusu kufanyika kwa maandamano mengine nchini humo.

Odinga na mrengo wake walisema maandamano hayo yanalenga kuishinikiza serikali ya Rais Ruto kuhakikisha kwamba inashughulikia suala la kupanda kwa gharama ya maisha. **RFI**



Miongoni mwa wananchi walioandamana akionekana akichoma moto matairi ikiwa ni moja ya vurugu zilizoshuhudiwa nchini Kenya katika maandamano ya upinzani yaliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# G20 yajadili unafuu wa madeni nchi maskini

**GANDHINAGAR,** INDIA

MAWAZIRI wa fedha na wakuu wa benki kuu katika nchi 20 zilizostawi kiviwanda na zinazoinuka kiuchumi G20, wameanza mazungumzo ya kurekebisha mikataba ya ulipaji madeni yanayozihusu nchi maskini.

Ilielezwa kuwa mazungumzo hayo yanayoendelea huko Gandhinagar India, pia yatakuwa yanajikita katika makubaliano yenye usawa, ya kodi za kimataifa kwa lengo la kuinua uchumi wa dunia.

Mkutano huo wa siku mbili, unaongozwa na waziri wa fedha wa India, Nirmala Sitharaman, anayesema, eneo linalotarajiwa kuwa na majadiliano mapana ni hali ya uchumi wa dunia.

Pia ilielezwa kuwa jambo la muhimu litakalokuwa katika ajenda hiyo ya siku mbili ni juhudi za kukabiliana na dhiki ya ulipaji madeni, huku nchi masikini zaidi duniani zikiathirika zaidi na mzozo wa madeni duniani, katika wakati ambao nchi hizo zinahitaji fedha zaidi kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Maofisa walibainisha kuwa China, ambayo ndiyo nchi yenye uchumi wa pili kwa ukubwa duniani na mkopeshaji mkubwa wa fedha kwa nchi kadhaa maskini barani Afrika na Asia, imekataa makubaliano yoyote ya pamoja yatakayoafikiwa kuhusiana na suala hilo la kurekebisha madeni, huku ikikosolewa mno kwa msimamo huo.

Akizungumza pembezoni mwa mkutano huo wa G20, waziri wa fedha wa Marekani, Janet Yellen, alitoa mfano wa urekebishaji wa deni la Zambia, jambo alilolizungumzia alipokuwa ziarani Beijing mwezi huu. Yellen alisema majadiliano kuhusiana na deni la Zambia yamechukua muda mrefu na kwamba anatarajia mazungumzo kuhusu madeni ya Ghana na Sri Lanka yatakamilika hivi karibuni.

Waziri huyo pia alishauri msingi uliotumika katika kurekebisha deni la Zambia utumike katika madeni mengine yote, badala ya kuanza mwanzo kwa kila nchi inayojadiliwa.

Aliongeza kwamba zaidi ya nusu ya nchi zote zenye kipato cha chini zinakaribia au tayari zishaingia katika matatizo ya ulipaji madeni, hiyo ikiwa ni mara mbili ya hali ilivyokuwa mwaka 2015, kauli iliyoungwa mkono na ofisa mmoja mwandamizi kutoka kwa mwenyeji wa mkutano huo India.

Aidha, ilielezwa kuwa G20 pia zitajadili mabadiliko ya taasisi za kimataifa za fedha, sarafu za kidijitali na mikakati ya kurahisisha upatikanaji wa fedha kwa nchi maskini, kwa ajili ya kukabiliana na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Hatua mpya ya kwanza kuhusiana na usambazaji wa mapato yanayotokana na kodi kutoka kwa makampuni yaliyo na matawi katika nchi nyingi, iliyofikiwa na nchi 138 wiki iliyopita, inatarajiwa kutangazwa katika mkutano huo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa makampuni ya teknolojia, kwa sasa yanaweza kuhamisha faida zao kwa urahisi katika nchi zilizo na viwango vya chini vya utozaji kodi, licha ya kuwa kiwango cha biashara cha makampuni hayo katika nchi hizo ni kidogo.

Vile vile, ilibainishwa kuwa kuna hofu kuhusiana na hatua ya nchi saba zilizostawi kiviwanda G7 kuvipa kipaumbele vita vya Russia na Ukraine, na kwamba ni jambo linaloweza kusababisha makubaliano ya mwisho kutofikiwa. **DW**

# AZAM KUPIGA TANO ZA KIRAFIKI TUNISIA, KUIVAA ESPERANCE J'5

**Na Abdallah Mataka**

BAADA ya kucheza mechi ya kwanza ya kirafiki ya kimataifa kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan nchini Tunisia, kesho, Jumatano Azam FC itajipima tena uwezo kwa kucheza na Esperance ya Tunisia.

Azam FC ambayo imeweka kambi nchini Tunisia ya kujiandaa na msimu mpya, katika mechi hiyo ya kwanza dhidi ya Al Hilal ilishinda mabao 3-1.

Akizungumza kwa njia ya simu kutoka Tunisia jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, alisema kocha wa kikosi hicho, Youssoupha Dabo, amepanga kutumia mechi hizo kukiimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa 2023/24.

Ibwe alisema baada ya mchezo huo, timu hiyo itacheza na US Monastir, Etoile Du Sahel na CS Sfaxien ambazo zote zinashiriki Ligi Kuu ya Tunisia.

Alisema Dabo anahitaji kutengeneza kikosi bora na ndio sababu ya kuhitaji mechi nyingi za kujipima nguvu katika kambi hiyo.

"Unajua kocha ni mgeni kuweza kuwazoea wachezaji, kwa hiyo ili kupata kikosi cha kwanza ilikuwa lazima kucheza mechi nyingi za kirafiki aweze kukijenga kuwa bora kwa msimu ujao," alisema Ibwe.

Alisema kocha wao anaendelea kukifua vema kikosi hicho ili kuwa tishio na kutimiza malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao pamoja na kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa.

Azam FC ambayo iliyoondoka nchini Julai tisa huku ikitarajia kurejea Julai 30, mwaka huu, itaiwakilishi Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika sambamba na Singida Fountain Gate FC huku Simba na Yanga zikiwa na jukumu hilo upande wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Itakaporejea nchini, itakuwa na kibarua kigumu dhidi ya Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga kwenye nusu fainali ya Ngao ya Jamii, mchezo utakaopigwa Agosti 9, mwaka huu katika Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

MAZOEZI...



Timu ya wasichana inayolelewa na Kituo cha Kukuza Vipaji cha Jk Park, wakifanya mazoezi katika viwanja vya kituo hicho jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BMT yaanika bajeti yake mpya

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limetoa tathmini yao ya mwaka wa fedha uliopita, kwa kueleza kuwa katika kipindi hicho ilitumia shilingi bilioni 4.2 kuziwezesha timu za taifa kushiriki katika mashindano ya kimataifa huku mwaka huu likitarajia kutumia zaidi ya bilioni tano.

Akizungumza Nipashe jana, Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha, alisema malengo yao yametimia ingawa kulikuwa na changamoto kadhaa katika kuandaa mashindano mbalimbali.

Alisema mwaka unaokuja watahakikisha wanafanya vizuri na kurekebisha changamoto ambazo zilitokea mwaka uliopita wa bajeti ili kuhakikisha michezo inaleta maendeleo nchini.

"Pamoja na kugharamia timu za taifa, lakini tulitoa tuzo kwa wanamichezo ambao walifanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na tuliandaa matamasha mawili ya wanawake moja riadha na Tanzanite.

"Tuzo za wanamichezo zitakuwa endelevu kwa ajili ya kuwapa motisha wachezaji, tunatarajia kuzindua mfumo wa kujisajili kwa njia ya mtandao ambao yote ni mafanikio ya mwaka wa fedha, kwa mwaka huu wa fedha tunatarajia kutumia zaidi ya shilingi bilioni tano," alisema.

Msitha alitoa wito kwa vyama na mashirikisho kuhakikisha wanatafuta wadau wa kusaidia klabu na mashirikisho yao katika maandalizi ya mashindano na kuzisaidia timu.

Aidha, katibu huyo alisema mafanikio waliyoyapata ni kutokana na uongozi mzuri wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha michezo inapiga hatua na wanamichezo wanapewa sapoti ili wafanye vizuri katika mashindano yao.

Wakati huo huo, Msitha alikabidhi bendera Timu ya Taifa ya Kuogelea na kuwataka wachezaji kuhakikisha wanaiweka nchi sehemu ya rekodi za dunia katika ushiriki wa mashindano hayo ambayo yataanza Julai 25, mwaka huu nchini Japan.

## Kinondoni yatisha Wazazi Super Cup

**Na Pilly Kigome**

TIMU ya soka ya Jimbo la Kinondoni imeanza vema mashindano ya Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Dar es Salaam ambayo yanajulikana kama Wazazi Super Cup, baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya timu ya Jimbo la Ubungo katika mchezo uliopigwa viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi.

Awali, kabla ya mechi hiyo kuanza, ilishuhudiwa timu ya Wazazi Vetenari ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya timu ya Wenyeviti wa Serikali za Mtaa katika mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo inayoshirikisha timu 10.

Timu zingine zinazoshiriki michuano hiyo ambayo inatarajiwa kumalizika Agosti 6, mwaka huu ni Jimbo la Ilala, Segerea, Ukonga, Temeke, Kigamboni, Mbagala, Kawe na Kibamba.

Mshindi wa kwanza katika mashindano hayo atajinyakulia zawadi ya shilingi milioni tano na medali 30 za dhahabu huku wa pili akiondoka shilingi milioni tatu na medali 30 za shaba na wa tatu akizawadiwa shilingi milioni 1.5 na medali za shaba.

Akizungumza katika ufunguzi wa mashindano hayo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Dar es Salaam, Hadija Saidi, alisema mashindano hayo yana lengo la kuwakutanisha wazazi pamoja na kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika suala zima la malezi.

## Michuano ya Gofu Majeshi Oktoba USA

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Majeshi ya mchezo wa Gofu yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Oktoba 10, mwaka huu nchini Marekani, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Klabu ya Lugalo ya Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ), Kanali David Mziray, alisema wanaendelea kuwanoa wachezaji wao ili wakaiwakilishe vema nchi katika mashindano.

"Mashindano ya wazi ambayo yalifanyika Moshi mkoani Kilimanjaro yamewasaidia wachezaji wetu kuendelea kupata uzoefu huku wakijiandaa na mashindano hayo ya Oktoba mwaka huu," alisema Kanali Mziray.

Alisema mwishoni mwa mwezi huu watashiriki mashindano kama hayo yatakayofanyika Mufindi mkoani Iringa ikiwa ni mwendelezo wa maandalizi yao.

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ATAKIWA LIVER

KLABU ya Liverpool inatazamia kumnunua kiungo wa Manchester City na England, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 27, wakati Fabinho anakaribia kuhamia Saudi Arabia. (***Mirror***)

### PALHINHA KUTUA WEST HAM

WEST Ham iko kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 27 kutoka Fulham. (***Talksport***)

### MCTOMINAY KUUZWA

ERIK ten Hag yuko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 25, ili kumudu uhamisho wa majira ya joto. (***Metro***)

### MORATA ATAKIWA INTER

BAADA ya kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kumnasa mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, Inter Milan wameelekeza macho yao kwa mshambuliaji wa Atletico Madrid mwenye umri wa miaka 30, Alvaro Morata na mshambuliaji wa Arsenal mwenye umri wa miaka 22, Folarin Balogun. (***La Gazzetta***)

### LUKAKU BASI TENA

ROMELU Lukaku hatasafiri katika ziara ya Chelsea ya kujiandaa na msimu mpya, huku kipaumbele chake kikiwa ni kumuuza kwa pauni milioni 34. Usajili wa Juventus unategemea mkataba kati ya mshambuliaji wa Paris St-Germain na Mserbia Dusan Vlahovic, 23. (***Fabrizio Romano***)

### DE GEA HUYOOO SAUDIA

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 32 anatarajiwa kuhamia Saudi Arabia baada ya mlinda mlango huyo wa zamani wa Hispania kupokea ofa nyingi kutoka kwa zaidi ya klabu moja. (***Daily Star***)

### CELSO AWANIWA NAPOLI

KIUNGO wa kati wa Argentina, Giovani lo Celso mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kuondoka Tottenham Hotspur huku Napoli wakianzisha mazungumzo kwa ajili ya mchezaji huyo. (***Daily Mail***)

### NASCIMENTO AWINDWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest ina nia ya kukamilisha usajili wa mshambuliaji wa Brazil, Matheus Nascimento mwenye umri wa miaka 19, kutoka Botafogo. (***UOL***)

### TAH KUBAKI LEVERKUSEN

LICHA ya West Ham kuonyesha nia ya kutaka kumnunua beki wa Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 27, mchezaji huyo anatazamia kusalia katika Klabu ya Beyer Leverkusen inayoshiriki Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga. (***Kicker***)

### PALMER AGOMBEWA

KLABU za Leicester City na Burnley zinatazamiwa kukutana ana kwa ana katika mpango wa kumsajili kwa mkopo kiungo mshambuliaji, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 21 kutoka Manchester City. (***Leicestershire Live***)

### BAILLY, TELLES KUUZWA

MLINZI wa Ivory Coast, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 29 na beki wa Brazil, Alex Telles (30), walishindwa kufika siku ya kwanza ya mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wa Manchester United huku kukiwa na mipango ya kuuzwa. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG AMVUA MAGUIRE UNAHODHA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

### Mwenyewe amshukuru Ole Gunnar Solskjaer, Fernandes sasa anukia kupewa kitambaa...

HARRY Maguire amevuliwa unahodha wa Manchester United na kocha, Erik ten Hag.

Mlinzi huyo wa England alikuwa nahodha wa 'Mashetani Wekundu' hao tangu Januari 2020, lakini hakupewa muda mwingi wa kucheza msimu wa kwanza wa Ten Hag kuongoza timu hiyo muhula uliopita.

**Maguire mwenye umri wa miaka 30, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Baada ya mazungumzo na kocha leo (jana) ameniarifu anabadilisha nahodha.**

"Alinieleza sababu zake na ingawa mimi binafsi nimevunjika moyo sana, nitaendelea kujitolea kila ninapovaa jezi ya timu hii.

"Kwa hiyo nilitaka kusema asante sana kwa mashabiki wa Manchester United kwa sapoti yao nzuri wakati nimekuwa nikivaa kitambaa hiki.

"Tangu siku nilipochukua jukumu hilo, miaka mitatu na nusu iliyopita, imekuwa ni bahati kubwa kuiongoza Manchester United na mojawapo ya nyakati za kujivunia maishani mwangu hadi sasa.

"Ni moja ya heshima kubwa katika soka la klabu. Nimefanya kila niwezalo kusaidia United kupata mafanikio - ndani na nje ya uwanja.

"Siku zote nitamshukuru Ole Gunnar Solskjaer kwa kunipa jukumu hilo kwanza na ninamtakia yeyote atakayechukua hatua hiyo kwa kila mafanikio na watakuwa na msaada wangu kamili."

Mustakabali wa muda mrefu wa Maguire kwa Mashetani Wekundu hao unabakia shakani baada ya kuanza mara nane pekee kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita.

Raphael Varane na Lisandro Martinez walikuwa chaguo la kwanza kwa Ten Hag kwenye safu ya ulinzi ya kati, pamoja na Luke Shaw akicheza kushoto.

Beki huyo wa kati wa zamani wa Leicester na Hull City amekuwa akihusishwa na uhamisho wa mkopo kutoka Old Trafford, huku West Ham wakiripotiwa kumtaka.

Kiungo Bruno Fernandes anaonekana ndiye anayetarajiwa kutwaa kitambaa cha unahodha baada ya kukivaa mara kwa mara wakati wa kukosekana kwa Maguire msimu uliopita.

HABARI MICHEZO

# Rooney amtabiria magumu Messi MLS

**MIAMI,** Mrekani

KOCHA wa D.C. United, Wayne Rooney, amesema Lionel Messi "hataona jambo rahisi" katika Ligi Kuu ya Marekani (MLS), baada ya kujiunga na Inter Miami.

Katika mahojiano na gazeti la The Times la London, mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United, Rooney alisema wachezaji wengi wanafika MLS na wanatatizika kuzoea na kwamba Messi anaweza kuwa hana tofauti.

"Kila kitu kimewekwa kwa ajili yake," alisema Rooney.

"Wenzake (Sergio) Busquets na Jordi Alba wamesaini Inter Miami na huenda (Andres) Iniesta akajiunga nao. Luis Suarez pia. Messi ana kocha (Miami Tata Martino) anayempenda na kumwamini.

"Hatapata jambo rahisi hapa. Inasikika kuwa wazimu, lakini wachezaji wanaoingia wanakuta ni ligi ngumu. Kusafiri, hali tofauti katika miji tofauti, na kuna nguvu nyingi na nguvu uwanjani."

Baada ya kuondoka United baada ya miaka 14, Rooney aliichezea D.C. United mechi 52 katika kipindi cha miaka miwili kuanzia 2018 hadi 2020, akifunga mabao 25, kabla ya kurejea kama kocha Julai mwaka jana.

Messi alitambulishwa katika hafla iliyofanyika kwenye Uwanja wa DRV PNK wa Inter Miami huko Fort Lauderdale, Florida juzi, Jumapili.

Mshambuliaji huyo wa Argentina anajiunga na Miami baada ya kuachana na mabingwa wa Ufaransa, Paris Saint-Germain baada ya misimu miwili katika klabu hiyo. Ametia saini mkataba hadi mwisho wa msimu wa 2025.

Klabu hiyo imesema Messi atacheza mechi ya kwanza Julai 21, mwaka huu, ya Kombe la Ligi dhidi ya Cruz Azul ya Mexico.







# BUSQUETS ATUA INTER MIAMI

**MIAMI,** Marekani

KLABU ya Inter Miami imethibitisha kumsajili mchezaji huru Sergio Busquets baada ya kumaliza mkataba wake na Barcelona.

Busquets alitumia misimu 15 katika kikosi cha kwanza cha Barca kabla ya kuondoka mwishoni mwa Juni mwaka huu, na kushinda mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, saba ya Copa del Rey na tisa ya Ligi Kuu ya Hispania, La Liga - likiwamo moja la mwaka wake wa mwisho katika klabu hiyo - wakati wa maisha yake ya soka na 'La Blaugrana' hao.

Kiungo huyo wa kati sasa ameungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Barca, Lionel Messi huko Miami.

Akizungumza baada ya kuhamia huko, kupitia tovuti rasmi ya klabu, Busquets alisema: "Hii ni fursa maalum na ya kusisimua ambayo ninafurahia sana kuichukua. Natarajia hatua hii inayofuata katika kazi yangu na Inter Miami.

"Nilifurahishwa na klabu nilipokuja na Barcelona mwaka jana na sasa nina furaha na niko tayari kuwakilisha klabu mwenyewe. Siwezi kusubiri kusaidia kuleta mafanikio ambayo klabu hii kabambe inapigania."

Mmiliki Mkuu wa Inter Miami, Jorge Mas pia alielezea furaha yake kupata mkataba huo: "Nina furaha kumkaribisha Sergio Busquets hapa Inter Miami. Tangu siku ya kwanza tumedhamiria kuleta wachezaji bora duniani Inter Miami. Sasa ripoti inajieleza yenyewe."

# Onana mali ya Man United

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United rasmi imefikia makubaliano na Inter kumsajili mlinda mlango, Andre Onana, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Cameroon, jana alitazamiwa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya kukamilisha uhamisho wa euro milioni 50 kwenda Old Trafford.

United wana matumaini Onana, ambaye atachukua nafasi ya David De Gea kama namba moja wa klabu hiyo, pia atapatikana katika safari ya kikosi chao kwa ajili ya ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, itakayoanzia jijini New York wiki hii.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mara Onana atakapokuwa rasmi mchezaji wa United, Dean Henderson, atapewa ruhusa ya kujiunga na Nottingham Forest kwa uhamisho wa kudumu.

Henderson alitumia msimu uliopita kwa mkopo Forest, na ingawa amerejea pale Carrington kwa ajili ya kuanza mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya, anatarajiwa kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 20 kwenda kule kwenye Uwanja wa City Ground.

Onana, ambaye alifanya kazi na Erik ten Hag wakati walipokuwa pamoja Ajax Amsterdam, atakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na United majira haya ya joto baada ya kuwasili kwa kiungo Mason Mount kutoka Chelsea.

Ataziba pengo la De Gea, ambaye ameondoka Old Trafford kwa uhamisho huru baada ya miaka 12 katika klabu hiyo.



# MOALLIN AIPELEKA KMC ZNZ KUSAKA UBANI WA LIGI KUU

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya Manispaa ya Kinondoni, KMC FC kimeondoka na tayari kimetua visiwani Zanzibar jana mchana kwa lengo la kuweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdulhamid Moallin, alisema kambi hiyo itasaidia kuwajenga vema wachezaji wao kuelekea msimu mpya wa 2023/24.

"Lengo la kwenda kuweka kambi visiwani humo tunataka kupata matokeo mazuri kwenye michezo yetu ya msimu ujao na kujiepusha kucheza mechi za 'play off' (mchujo) kuwania kubaki Ligi Kuu," alisema.

Alisema wakiwa visiwani Zanzibar watatafuta timu za kucheza nazo michezo ya kirafiki ambayo aanamini itamsaidia kuangalia uwezo na mapungufu ya kila mchezaji.

Moallin aliwaomba mashabiki pamoja na wadau wa timu hiyo kumuunga mkono ili aweze kutimiza malengo waliyojiwekea.

"Nitahakikisha naipambania timu yangu ili ishike nafasi ya juu msimu ujao ambao naamini utakuwa na ushindani mkubwa, hivyo ninaomba mashabiki wanipe ushirikiano," alisema.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kitunda jijini Dar es Salaam, wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya shule hiyo hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sababu Chama kusalimu amri Simba

INATOKA UK 24

akifanya hivyo karibuni kila msimu, Rais wa Heshima wa Klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, akaandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram: "Huyu mchezaji mkubwa ambaye ana mkataba na timu kubwa, mbona analeta tabu, Simba ikiamua jambo imeamua."

Huku mashabiki wa soka, wachambuzi, wanachama na mashabiki wa Simba Wakitafakari chapisho hilo, muda mfupi baadaye ndipo ilipotoka taarifa ya uongozi kumalizana na mchezaji huyo.

"Chama na Ngoma muda wowote kuanzia sasa [jana], wataanza safari kwenda kwenye kambi yetu nchini Uturuki," ilieleza taarifa hiyo.

Habari kutoka ndani ya Klabu hiyo zinasema kuwa sakata hilo lilianza baada ya kurejea kutoka nchini kwao Zambia akitaka kuongezewa maslahi ambayo kimsingi hayamo kwenye mkataba.

"Alikuwa kwao Zambia, aliporejea akasema mkataba wake umekwisha anataka kuondoka na hii ni kwa sababu alidhani hatujaingiza pesa yake iliyobakia ya usajili na hii imo kwenye mkataba, tukamwambia akaangalie salio lake benki, alipoona tumemuingizia hivyo mkataba bado unasoma akaanzisha madai mengine, mara anataka kuvunja mkataba, mara anataka aongezewe kiasi cha pesa ambacho alidai kwamba aliahidiwa tu kwa mdomo na mmoja wa viongozi aliyepita, ndiyo anayoing'ang'ania, lakini haipo kwenye maandishi," kilisema chanzo hicho.

Chanzo hicho kimesema pia Chama alishawaambia kuwa amepata ofa, lakini walipomuuliza ni klabu gani na kuitaka iende mezani na kuzungumza nao alikataa kuitaja.

Baada ya kuona usumbufu unazidi, viongozi wa Simba walimwambia avunje mkataba kwa kutoa Dola za Kimarekani milioni moja sawa na zaidi ya Sh. bilioni 2.4 za Tanzania, kama kifungu cha mkataba kinavyosema ili aondoke, au klabu yoyote inayomtaka ije mezani kitu ambacho kilimtoa jasho na kuwa kigumu kwake kukitekeleza.

Wakati huo huo, kundi la pili la wachezaji wa klabu hiyo liliondoka usiku wa kumkia jana kwenda Uturuki kuungana na wenzao kambini.

Kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, walioondoka ni Jean Balake, Che Fondoh Malone na Willy Onana ambapo watakapofika jijini Ankara watakutana na mchezaji mwingine Aubin Kramo na kuungana kabla ya kuelekea kambini, huku kundi la tatu linaliotarajiwa kuongozwa na Chama na Ngoma likitarajia kuondoka muda wowote kuanzia jana.

Katika hatua nyingine, Nipashe limepenyesewa taarifa kuwa winga hatari wa zamani wa timu hiyo, Luis Miquissone, dili lake la kurejea Msimbazi limekamilika na kwamba mchezaji atakayempisha ni Msenegal Pape Sakho.

Baada ya dili hilo kukamilika Simba sasa iko mbioni kumuuza Sakho anayewaniwa na klabu kutoka Ubelgiji na Ufaransa.

Awali, Simba ilienda Al Ahly kumuomba mchezaji huyo kwa mkopo ambao utakuwa na makubaliano ya kulipa mshahara wa Sh. million 25 huku ikiitaka timu yake hiyo Sh. milioni 55, kitendo ambacho kiligomewa na timu hiyo kabla ya Simba kukaa upya na mshambuliaji huyo kuweza kukamilisha suala hilo.

Alipoulizwa Ahmed, alisema: "Ni kweli suala la Miquissone sasa huenda likawa limeisha kwa sababu mchezaji mwenyewe na uongozi washamalizana kila kitu na kilichobaki kwa sasa ni mazungumzo kati ya Al Ahly ili kuona wanaweza vipi kukamilisha usajili huo wa mkopo kabla ya kuanza kwa msimu upya."

# Namungo kuzindua jezi leo, yataja bei

**Na Abdallah Mataka**

KLABU ya Namungo inatarajia kuzindua jesi zake za msimu wa 2023/24, leo huku ikijipanga kumaliza Ligi Kuu msimu huo ikiwa ndani ya nafasi nne za juu.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Namungo FC, Mbaruka Mtopea, alisema mwaka huu hawatarudia makosa ambayo yalitokea msimu uliopita kwani iliwalazimu kucheza mechi kadhaa na jezi za zamani kabla ya kuzindua jezi mpya .

"Tumejifunza kutokana na makosa ambayo yalitokea msimu ulioisha, tumejipanga kuhakikisha tunazindua vifaa vyetu vya michezo mapema," alisema.

Mtopea alisema wanategemea kuuza jezi hizo kwa bei ambayo itakuwa rafiki kwa kila shabiki wa Namungo FC kumudu kununua.

"Jezi zetu zitauzwa kwa gharama ya Sh. 20,000 ambayo tunaimani kila shabiki wa Namungo ataweza kumudu kuwa na uzi huo," alisema.

Namungo imekosa nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu baada ya kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Katika kuhakikisha inawania nafasi hiyo kuelekea msimu mpya inakwenda kuweka kambi mjini Karatu kujiandaa kwa Ligi Kuu inayotarajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu.

# Mayele avuta wanne Yanga

INATOKA UK 24




Abdallah raia wa Burundi ambaye ni chaguo la pili akiwa amemaliza mkataba wake na Klabu ya Kuching FC ya Malaysia.

Mchezaji wa nne ni William Karamako mwenye umri wa miaka 19 tu, akichezea Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amebainisha kuwa mpaka sasa klabu yao haijatoa taarifa rasmi kuhusu jambo hilo, lakini amesema mazungumzo yamefanyika vizuri na maamuzi yatatolewa hivi karibuni.

# Michezo

Nipashe Jumanne Julai 18, 2023

UK. 21

Ten Hag amvua Maguire unahodha UTD

# Sababu Chama kusalimu amri Simba

## ●●●Bilioni 2.4/- zatajwa kumtoa jasho, Miquissone naye kupishana na Sakho baada ya...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya majadiliano na mvutano wa hapa na pale na viongozi wa Simba, hatimaye kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous Chama 'Mwamba wa Lusaka', amesalimu amri na anatarajia kuondoka nchini muda wowote kuelekea Uturuki kujiunga na wenzake kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao unaotajiwa kuanza Agosti 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Klabu ya Simba jana jioni,baada ya majadiliano na mambo kuwekwa sawa, mchezaji huyo sasa ataungana na kundi la tatu likiongozwa mchezaji mpya, Fabrice Ngoma kuelekea Uturuki.

Hata hivyo, taarifa za ndani za kikao zilizotufikia ni kwamba Chama mwenye mkataba na Simba hadi mwaka 2024, ataongezewa mshahara kwa mwezi baada ya kusaini mkataba mpya utakaomuweka klabuni hapo hadi mwaka 2026.

Kabla ya makubaliano hayo kutangazwa jana jioni, wanachama na mashabiki wa Simba kwenye mitandao ya kijamii tangu asubuhi walionekana kukasirishwa na kitendo cha mchezaji huyo kubaki nchini wakati wenzake wakiwa nchini Uturuki kwenye 'pre season', wengine wakienda mbali wakitaka apewe adhabu kali, au atimuliwe.

Wakati wakiendelea kuushinikiza uongozi kuchukua hatua kwa mchezaji huyo kwa madai amekuwa

INAENDELEA UK 23



Lilepo

# Mayele avuta wanne Yanga

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KUKAMILIKA kwa dili la kumuuza mshambuliaji Fiston Mayele kwenda Pyramids ya Misri, kumeifanya Yanga kutupa ndoana kwa washambuliaji wanne ikilenga kumpata mmoja ambaye viatu vya Mkongomani huyo vitamtosha vizuri.

Mayele ameondoka Jangwani akiwa na rekodi ya kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara akiwa na mabao 17 huku pia akichukua kiibuka mfungaji bora kwenye Kombe la Shirikisho Afrika kwa kucheka na nyavu mara saba.

Kwa mujibu wa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, zemeleza tayari Yanga imefanya mazungumzo na straika Masoud Juma Choka, anayeichezea Klabu ya Difaa El Jadida ya Morocco, ambaye alikuwa kwa mkopo kwenye kikosi cha Al-Faisaly FC ambapo msimu uliopita alicheza jumla ya michezo 13 na kufunga mabao nane.

Nyota huyo ambaye amepita kwenye timu kadhaa za Sonny Sugar, Kariobangi Sharks Cape Town City, Dibba Al Fujairah, Al-Nasr Benghazi, JS Kabylie, rekodi za Choka akiwa na Difaa El Jadidi tangu alipojiunga nayo mwaka 2020, amecheza jumla ya michezo 56 na kufunga mabao 16.

Mshambuliaji mwingine anayehusishwa na Yanga kwa mujibu wa chanzo chetu ni Makabi Lilepo, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anayecheza Klabu ya Al Hilal Omdurman ya Sudan.

Habari zinasema Lilepo, mmoja wa mastraika hatari Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati anayeichezea Al Hilal ya Sudan akiwa ndiye chaguo la kwanza, na mwingine ni

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042